ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Piliwa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri waNchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma naUtawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando

13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga

29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
32.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasiza Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni

52.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
54.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
55.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
56.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
57.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
59. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
62.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
63.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
64.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
66.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
69.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
70.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe

75.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Thalathini na Moja – Tarehe 27 Julai, 2012

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha rasmi mezani hati ya Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuhusu Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Fedha ya mwaka 2012/2013. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, ahsante sana. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari.

Mhe. Asha Bakari Makame (Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari): Mhe. Spika, kabla ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye ametuwezesha kufika hapa leo katika hali ya uzima na baadaye nikuchukuru wewe kunipatia nafasi hii asubuhi.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hati mezani ya Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2012/2013. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa Fedha 2012/2013 –
Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo

(Majadiliano Yanaendelea)

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nichukue nafasi tena kama kawaida kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote pamoja na mawaziri kwa kujenga mashirikiano makubwa ya kuendesha shughuli zetu za Baraza hili kwa ajili ya wananchi. Kwa kweli ni mwenendo mzuri unatusaidia kufanikisha malengo ambayo serikali inakusudia kuyafanya, kwa ajili ya maendeleo ya wananchi kupitia wizara mbali mbali.

Vile vile nashukuru kwa maelekezo aliyotoa Mhe. Mwenyekiti jana kwamba kutokana na hali ya muda ulivyo tusingeweza kuendelea na majadiliano, kwa kiasi fulani ninayo taarifa kwamba mlipokea jambo hilo Waheshimiwa Wajumbe licha kwamba kulikuwa na orodha kubwa kidogo, ambayo mlitaka kuendelea kuichangia kama alivyoomba waziri kwamba achangiwe, lakini kwa ufinyu wa nafasi ikawa hali hiyo ni ngumu.

Kwa hivyo, nichukue nafasi hii sasa sina hakika Mhe. Naibu Waziri kama yupo, inaonekana hayupo. Lakini nimkaribishe moja kwa moja Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Karibu sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adhimu na muhimu sana, katika kutoa majumuisho ya michango ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuhusiana na makadirio ya bajeti ya wizara yangu.

Vile vile niendelee kukushukuru Mhe. Spika, kwa namna unavyoliendesha Baraza letu, kwa kweli wananchi wote wa Zanzibar wamejenga imani sana na chombo hichi. Nakushukuru sana.

Mhe. Spika, naomba niwashukuru Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa michango yao, hakika wamenisaidia sana. Pia nikiri kwamba ilikuwa ni michango yenye kujenga tena nina imani itanisaidia sana katika usimamizi wa wizara hii. Kwa hivyo, niwaombe na wakubali kwamba binafsi wameninoa vizuri zaidi na niko tayari kwa kazi baada ya kupitisha bajeti hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sasa naomba niwatambue wale waliochangia bajeti ya wizara yangu kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Asha Bakari Makame (Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza lako Tukufu.
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.
3. Mhe. Nassor Salim Ali.
4. Mhe. Ashura Sharif Ali.
5. Mhe. Ismail Jussa Ladhu.
6. Mhe. Hija Hassan Hija.
7. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa.
8. Mhe. Mohammed Haji Khalid.
9. Mhe. Asaa Othman Hamad.
10. Mhe. Jaku Hashim Ayoub.
11. Mhe. Wanu Hafidh Ameir.
12. Mhe. Hamza Hassan Juma.
13. Mhe. Shadya Moh'd Suleiman, ambaye amechangia kwa maandishi.
14. Mhe. Farida Amour Moh'd.
15. Mhe. Abdalla Moh'd Ali.

Mhe. Spika, baada ya utambuzi huo, naomba kujibu hoja za Waheshimiwa Wajumbe kama ifuatavyo.

Mhe. Asha Bakari Makame (Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari). Kwa kweli naomba nimshukuru sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati yangu kwa hotuba yake na mimi, Mhe. Naibu Waziri pamoja na watendaji wangu zimetupa moyo sana. *(Makofi)*

Vile vile naomba kumhakikishia Mhe. Mwenyekiti pamoja na kamati yake nzima kwamba wizara yangu iko tayari kupokea maelekezo ya kamati na kuyafanyiakazi, kama ambavyo tumeyapokea yale ya Hoteli za Pemba na zile za ujengaji wa ukuta wa kuzuia mmong'onyoko wa fukwe kandokando ya Hoteli ya Bwawani. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nilihakikishie Baraza lako Tukufu, kwamba Hotuba ya kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kama ilivyosomwa na Mhe. Asha Bakari Makame akiwa Mwenyekiti wa Kamati tumeichukua na maagizo yake tutayafanyiakazi yote katika muda mfupi ujao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika hotuba ya Mwenyekiti kuna jambo ambalo amelitolea indhari na Mwenyekiti akitoa indhari basi kuna jambo amelitilia wasi wasi. Kwa hivyo, naomba kuchukua nafasi hii kumtoa Mhe. Mwenyekiti, Kamati yake pamoja na Wajumbe wengine waliozungumzia kuhusu suala la uhamishaji wa mnara kutoka Chumbuni kwenda Bungi kama ifuatavyo.

Mwishoni mwa mwaka jana serikali iliamua kuhamisha mnara wa Redio wa Chumbani kwenda Bungi, ili kurahisisha utuwaji wa ndege kwa usalama na kazi hiyo ilikuwa na sehemu nne.

Kwanza kulizungushia uzio eneo lote la Chumbuni lenye ukubwa wa hekta karibu 200 kwa ajili ya kudhibiti uvamizi na kazi hii imeshafanyika kwa asilimia mia moja. Pili kulizungushia uzio eneo lote la Bungi, ili kulidhibiti na uvamizi na kazi hii imeshafanyika kwa asilimia mia moja.

Tatu ilikuwa ni kujenga nyumba za wafanyakazi za familia nne Bungi, Afisi ya Walinzi Bungi, Ujenzi wa *Studio* Bungi, Kibanda cha *Generator* Bungi na kazi hii imekamilika kwa asilimia 90 na asilimia 10 iliyobakia ni shughuli za umeme.

Kazi ya nne ni kushusha mnara wenye urefu wa mita 125 Chumbuni na kuujenga umpya Bungi. Vile vile kuhamisha mitambo kutoka Chumbuni kwenda Bungi.

Mhe. Spika, urefu wa mnara huu ni kama nilivyosema ni mita 125 wenye vipande 21 vya mita 7 kila kimoja. Kazi ya kuteremsha mnara ilikamilika vipande vyote 21 na hadi jana vipande 18 tayari vimeshapandishwa juu bado vipande vitatu na nimeahidiwa vitapandishwa siku mbili zinazokuja.

Mhe. Spika, ni kweli hapo katikati shughuli za upandishwaji wa mnara zilisuasua kwa mizozo kati ya kampuni yenyewe na wafanyakazi wake. Kutokana na hali hiyo, mimi binafsi nikatoa agizo apelekewe *notice* ya kufikishwa Mahakamani kwa mujibu wa mkataba, mara baada ya kupata *notice* yangu alikuja ofisini na kuomba radhi na kujibu *notice* niliyompelekea na akaniahidi mnara utakuwa umekamilika hadi tarehe 31 mwezi huu.

Mhe. Spika, mimi mwenyewe binafsi nimeshakwenda Bungi mara 15 ndani ya kipindi hichi cha miezi mitatu na nimejenga matumaini kwamba ikifika tarehe 30 mwezi huu vipande vitatu vilivyobakia vitakuwa vimeshapandishwa juu. Kazi itakayobakia ni uhamishaji wa mitambo, ambapo nimeomba msaada wa Wahandisi kutoka *State Radio* ya China, ambao wameniahidi mwezi ujao wa August watafika kwa ajili ya kukamilisha kazi hiyo.

Mhe. Spika, naomba nimshukuru Mhe. Waziri Abdillah Jihad Hassan kwa kusimamia sehemu kubwa ya kazi hii na mimi nimekuja kutoa mchango wangu wa mwisho mwisho. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Mwenyekiti pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wengine waliozungumzia suala la Bungi, kwamba watupe imani na watuamini kuwa tukijaaliwa baada ya muda mfupi mnara utakuwa umeshafika juu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia Mhe. Makame Mshimba Mbarouk naye alitoa mchango mkubwa katika hotuba yangu, namshukuru kwa mchango wake amenisaidia sana. Kwa kweli huyu ni Mwenyekiti makini sana wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi wa Baraza lako Tukufu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa aligusia suala la maslahi ya wafanyakazi wa Kamisheni ya Utalii. Ni kweli Kamisheni ya Utalii ndio muhimuli wa uchumi wetu, wafanyakazi wake nawapaswa kuenziwa kimaslahi. Hili tumeliona na kupitia *Scheme of Service* itakayoundwa, basi nitahakikisha kwamba wafanyakazi wa Kamisheni ya Utalii maslahi yao yamekuwa juu. *(Makofi)*

Kuhusu bajeti ya *promotion* ni ndogo ni kweli kulinganisha na wenzetu majirani. Lakini hii ndio hali ya uchumi wetu na mgao wa fedha tunazozipata ukilinganisha na wenzetu jirani kwa kweli sisi bajeti yetu ya *promotion* ni ndogo sana. Mhe. Spika, mtu hujikuna ajipatapo na serikali imesikia na sisi tutaendelea kutumia kwa makini tulichonacho, ili kuona kwamba tunajitahidi kuitangaza nchi yetu.

Kikosi cha *Patrol Unity* ambacho Mhe. Makame Mshimba Mbarouk alikizungumzia kinaratibiwa na Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Kamisheni yangu ya Utalii.

Kuhusu Bodi ya Kamisheni ya Utalii bado haijaundwa, lakini itaundwa kwa sababu Mhe. Rais kama mwezi mmoja uliopita ndio alitia sahihi ile sheria na kwa hivyo baada ya bajeti hii kupitishwa tutahakikisha kwamba tunaharakisha kuiunda upya Kamisheni ya Utalii na Bodi yake.

Mhe. Spika, kuhusu wafanyakazi wa Hoteli ya Bwawani Mhe. Makame Mshimba Mbarouk pamoja na Waheshimiwa Wajumbe mbali mbali walizungumzia suala la mikataba ya muda ya miezi mitatu na sita kwa wafanyakazi wa Hoteli ya Bwawani.

Mhe. Spika, kwa kweli Waheshimiwa Wajumbe mimi ni mwenzao sana, hivyo ninawaomba sana wakipewa mambo yanayohusu wizara hii tuulizane. Kwa maana hiyo, inaonekana kuna kikundi cha watu kimewapa taarifa ambayo si sahihi Waheshimiwa wengi wa Baraza lako

Tukufu. Ukweli ni kwamba wafanyakazi wote wa Hoteli ya Bwawani 125 wana ajira ya kudumu tokea mwaka jana na huo ndio usahihi wake. *(Makofi)*

Vile vile Mhe. Makame Mshimba Mbarouk pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wengine pia walizungumzia kuhusu unyanyasaji wa wafanyakazi katika mahoteli ya kitalii. Mhe. Spika, jambo hilo halikubaliki na mimi kama waziri ambaye ninayesimamia Sekta ya Utalii niko tayari kupambana na mwekezaji yeyote mwenye tabia kama hizo, kwa sababu lazima wawekezaji wajue kwamba hii ni nchi ya Zanzibar na wazanzibari wenyewe tupo.

Kwa hivyo, ninachowaomba Waheshimiwa Wajumbe kwamba mambo haya yakitokea tuarifiane, ili Kamisheni ya Utalii pamoja na Kamisheni ya Kazi zipate nafasi za kuwachukuliwa wawekezaji wenye tabia mbaya kama hizo hatua mujarabu kwa mujibu wa sheria.

Aidha naomba nimpe pole sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* na Wajumbe wake kwa kudhalilishwa na mwenye hoteli hiyo. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Mwenyekiti mambo kama haya yakitokea basi tuarifiane, ili tuweze kuchukua hatua zinazostahiki.

Pia namuahidi Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kwamba niko tayari baada ya mwezi Mtukufu wa Ramadhani kupata nafasi kutembelea mahoteli yalioko kwenye jimbo lake, ili kuangalia hali ya ajira ya wananchi wake.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk vile vile alizungumzia Shirika la Utalii. Mhe. Spika, naomba niseme kwamba Shirika la Utalii uwepo wake ni wa mpito kuelekea ama kuvunjwa au kuimarishwa kutegemea na ripoti ya mtaalamu atakayoitoa ndani ya robo ya kwanza ya mwaka huu wa fedha wa 2012/2013.

Wizara iliajiri mtaalamu kulichunguza shirika, ili kuona vipi katika enzi hizi za kutembeza wageni sekta ambayo imedhiwa na watu binafsi juu ya shirika kwa rasilimali iliyonazo na mitaji iliyonayo inaweza kujiendeshaji kibiashara na kifaida. Je, tukilivunja rasilimali zake zirudishwe serikalini na zitumike vipi. Je, wafanyakazi 15 wa shirika maslahi yao yalipwe katika utaratibu upi?

Hayo ni mambo ambayo wizara tunayasubiri kuyapokea na tutayafikisha serikalini na hatimaye chombo hichi muhimu kitakuja kuarifiwa. Kwa hivi sasa mapato ya Shirika la Utalii inayokusanya yanatosha sana kulipa mishahara na marupurupu mengine kwa watumishi hawa 15.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk pia alizungumzia suala la Chama cha Riyadha ni kweli chama hichi hakijafanya uchaguzi wake. Baraza la Taifa la Michezo limesaidia kufanya Mkutano Mkuu wake wa maandalizi ya uchaguzi kwa mujibu wa Katiba yanaendelea vizuri. Kwa kweli Chama hichi cha Riyadha hakijatupwa na kinapewa fursa nyingi.

Aidha taarifa nilizonazo ni kwamba shilingi milioni 1,000,000/= kutoka kwa Rais Mstaafu walishakabidhiwa zamani ikiwa miongoni mwao hawana taarifa basi namuomba Mhe. Makame Mshimba Mbarouk aje nao wizarani, ili tufahamisheni vizuri zaidi.

Pongezi alizotoa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kwa Idara ya Makumbusho na maeneo mengine ya wizara yangu tunayapokea na tunamshukuru sana.

Mhe. Nassor Salim Ali kwanza nimshukuru sana kwa namna anavyonishauri na kunielekeza mara kwa mara katika shughuli mbali mbali za wizara yangu. Kwa kweli yeye huwa hasubiri Kikao cha Baraza wakati anapoliona jambo linahitaji usimamizi ama hulishughulikia au hunipata taarifa na kwa pamoja tukalishughulikia namshukuru sana.

Mhe. Spika, pongezi zake tumezipokea na kuhusu kujipanga kupata tunzo zaidi ya Sekta ya Utalii tumekusudia kuandaa mikakati ya *promotion* ya vivutio vyetu, kwa sababu Zanzibar ina vivutio vingi ambavyo ni *unique* na Kamisheni ya Utalii tumekusudia kuvitumia. Vile vile ushauri wake kukuza Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar kukipa hadhi pia tunauchukua na tunamshukuru.

Kuhusu maendeleo ya Soko la Wanawake ni kweli halijapata nguvu inayosatahiki. Tunaye Kocha Msaidizi wa Timu ya Wanawake Tanzania, ambaye ameahidi kushirikiana na uongozi mpya wa *ZFA* kwa ajili ya kuendeleza Soko kwa Wanawake.

Tatizo tulilonalo ni kwamba wanawake wa Zanzibar hawajapata hamu ya kushiriki katika mchezo huu, Baraza la Taifa la Michezo na Kamisheni ya Utamaduni na Michezo inakusudia kushirikiana na Wizara ya Elimu kulizungumzia suala hili kwa mujibu wa mila, silka na utamaduni wetu.

Mhe. Nassor Salim Ali pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wengine walizungumzia kuhusu suala la Kiwanja cha Amani. Mhe. Spika, ni kweli ile *peach* ya Uwanja wa Amani sio nzuri na inahitaji kushughulikiwa ipasavyo. Jitihada zilifanywa hapo nyuma kwa kupandwa majani hasa Mhe. Naibu Waziri wangu wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo alisimamia sana hili. Lakini tunalo tatizo kubwa la ukosefu wa maji katika eneo lile, kisima kilichimbwa na wala hayakupatikana maji yenyewe.

Kwa kweli kwa hali ya kiwanja kilivyo na umuhimu pamoja na historia yake kwa taifa mimi nimekusudia kufanya mambo mawili. Kwanza baada ya hali kuwa mbaya kiasi ya kwamba Simba na Azam kukataa kucheza kwenye uwanja huo, basi mimi nilimwita Mkurugenzi wa *FIFA* wa Miradi ya Maendeleo kwa Afrika kutoka Switzerland pamoja na Mkurugenzi wa Ufundi wa *TFF*, walikuja Zanzibar na tukenda nao Uwanja wa Amani tukaukagua na wakaniahidi mambo mawili.

Jambo la kwanza kuleta wataalamu wa *FIFA* kuja kufanya matengenezo ya dharura. Pili kuangalia uwezekano wa kuwekwa nyasi bandia mwakani na hizo ni jitihada za nje.

Mhe. Spika, kwa jitihada za ndani nimemuomba Mhe. Mohamedzara Hassanali Mohamedali mwanamichezo maarufu, mahiri, mzalendo na mwenye uchungu wa Zanzibar kuunda kamati itakayoshirikisha Rais wa *ZFA* Amani Ibrahim Makungu na Katibu wake na watu wengine tunaowaamini ambao tunao wengi, ili kuangalia namna gani Uwanja huo wa Amani utarudi katika hadhi yake.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali amenikubalia na ameniahidi kwamba baada ya muda mfupi tutakaa kikao cha kwanza kwa ajili ya kuamua namna gani tufanyekazi hiyo.

Mhe. Nassor Salim Ali pia alizungumzia kuhusu Kocha Abdul-Fatah kutoka Misri ni kweli alikuwa hatumiki vizuri. Lakini Uongozi mpya wa ZFA hasa Rais wake Amani Ibrahim Makungu amemshirikisha vizuri na ameanza kazi ya kufundisha vizuri Timu ya *Under twenty three, Under twenty and Seventeen*.

Mhe. Spika, kuhusu vifaa vya Timu ya *Cricket*, ambapo Mhe. Nassor Salim Ali alizungumzia nimefuatilia suala hilo na taarifa niliyopewa ni kwamba Mwenyekiti wa Chama hicho Bwana Juma Saadati amekubali kwamba alikabidhiwa vifaa hivyo na aliyekuwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo Mhe. Ali Juma Shamuhuna pamoja na Naibu Waziri wake Mhe. Mahmoud Thabiti Kombo na wamevitumia kwa ajili ya kuendeleza mchezo huo na baadhi ya vifaa hivyo wanavyo.

Mhe. Ashura Sharif Ali, kwa kweli Mhe. Spika, Mhe. Mjumbe alizungumzia juu ya kadhia ya wafanyakazi 7 waliofukuzwa au waliosimamishwa bila ya utaratibu.

Ukweli ni kwamba katika miezi yangu hii mitatu ya kuwepo wizarani sikuridhika na makusanyo ya mapato katika Shirika la *ZBC*, ndipo nilipoandaa utaratibu wa kuangalia namna gani ukusanyaji huo unafanyika katika *ZBC Radio*. Kwa hivyo, nilichogundua ni kwamba Matangazo ya Vifo yanayotangazwa kwenye redio ni mengi ukilinganisha na risiti za malipo zinazoandikwa kinyume na taratibu za fedha. *(Makofi)*

Pili malipo yanayokusanywa hubaki mfukoni na wala hayapelekwi katika Kitengo cha Ukusanyaji wa Fedha kwa wakati. Mhe. Spika, kwa mujibu wa Sheria za Fedha haya ni makosa makubwa na yangepaswa adhabu kubwa zaidi.

Lakini mimi nimeamua kwamba wahamishwe wote kutoka Kitengo cha Mapato na waekwe katika maeneo mengine. Kwa maana hiyo, hawajafukuzwa, isipokuwa wamepewa kwa sababu ya utaratibu wa kulinda fedha za nchi na nahakikisha kwamba Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* hili ataliunga mkono sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa maelezo hayo nadhani Mhe. Ashura Sharif Ali ataridhika na lile dai lake la kuzuia fungu letu sasa ataliachia.

Vile vile Mhe. Ashura Sharif Ali alihoji kuhusiana na kuhama kutoka *Analogy* kwenda *Digital* ifikapo tarehe 31 Disemba. Mhe. Spika, kama tulivyozungumza awali ni kwamba jitihada za kupata mkopo zinaendelea vizuri na wahandisi ya Kampuni ya ***HUAWEI*** ya China wamenihakikishia kwamba kwa vifaa tulivyonavyo wanahitaji mwezi mmoja tu kuifanya Zanzibar kupata asilimia 40 ya Mtandao wa *Digital* na miezi mingi michache baadaye kumalizia sehemu iliyobaki.

Kwa kweli jitihada inafanywa mimi, Wizara ya Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na serikali kwa jumla kuona kwamba tunapata fedha kwa ajili ya kuilipa Kampuni ya ***HUAWEI***, ili tuendeleze katika shughuli hiyo.

Mhe. Spika, ushauri juu ya kujipanga upya kuhusu utalii tumeuchukua na ndio mahitaji ya Sheria mpya ya Utalii iliyopitishwa na baraza lako Tukufu. Vile vile kuhusu Chuo cha Maendeleo ya Utalii na *NACTE* kuwa na usajili wa muda, kwa kawaida *NACTE* huwa hawatoi usajili wa mpigo moja kwa moja na huwa wana *stage* tatu.

Kwanza ni *Preparatory Registration*, kwenda kuangalia kama wanaweza kuwa *sustainable*. Pili *Provision Registration* miaka miwili wanaangalia mitaala, maktaba, *Strategic Plan*, sera na namna ya kuwahudumia walimu, wakiridhika na hayo ndio huwa wanatoa *Full Registration*.

Mhe. Spika, Chuo chetu ya Maendeleo ya Utalii Zanzibar hivi sasa kimepewa *Provision Registration* na Mkurugenzi wa Chuo amejitahidi sana na kukamilisha matakwa yote na wakati wowote atawaita waje wakague na tumaliziane na watupe *Full Registration* ya *NACTE*.

Mhe. Spika, ushauri wa Mhe. Ashura Sharif Ali kuhusu mila na utamaduni wa Mzanzibari tumeuchukua na tunaufanyiakazi. Vile vile kuhusu mikataba ya wafanyakazi wa Hoteli ya Bwawani ni kama nilivyomjibu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Mhe. Hija Hassan Hija Mwakilishi makini wa Jimbo la Kiwani namshukuru sana kwa michango yake na yeye alizungumzia kuhusu unyanyaswaji wa Wazanzibari kwenye mahoteli. Kwa hivyo, naomba aridhike sana na majibu niliyoyatoa kwa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kuhusiana na kadhia hii na niliahidi Baraza hili kwamba nikipewa taarifa kwa wakati, basi tutawashughulikia inavyopaswa.

Vile vile Mhe. Mjumbe alizungumzia kuhusu suala ufanizi mdogo wa Shirika la *ZBC*. Mhe. Spika, naomba nikiri na ni kweli hatujapata ufanisi tunaouhitaji katika shirika hili. Tumeanza kubadilika katika hali ngumu na tunashukuru wale wote wanaotupa moyo kwamba mabadiliko yanaonekana katika Shirika la *ZBC*.

Mhe. Spika, Shirika la *ZBC* sio tu halina betri ya gari, mpira wa gari, mafuta ya gari, lakini pia maslahi ya wafanyakazi wake ni duni sana dhidi ya kazi nzito wanayoifanya na huo ndio ukweli wenyewe. Lakini vifaa muhimu kama vile *mixer*, *camera* za kileo, vifaa vya kutengenezea vipindi na hata *AC* hatuna pamoja na taaluma ya mafundi, watangazaji, watayarishaji vipindi na hata viongozi wenyewe wa Shirika inahitaji kuongezwa.

Mhe. Spika, sisi kama viongozi wa wizara tumeuona udhaifu huo na tumekaa na serikali na tumekubaliana kuunda Tume ya Wataalamu wenye uzoefu katika Sekta ya Habari. Tume hiyo imeshaundwa na kazi hiyo wanaifanya kwa muda wa mwezi mmoja na tarehe 30 mwezi huu tunatarajia kupokea na kutushauri juu ya uongozi, muundo, ufundi, utangazaji, uendeshaji pamoja na maslahi ya wafanyakazi. Kwa hivyo, ninachomuahidi Mhe. Mjumbe ni kwamba *ZBC* lazima ibadilike na tutaisimamia ibadilike. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nilipoingia wizarani miezi mitatu iliyopita nilikuta malimbikizo makubwa ya madai ya wafanyakazi. Kwa hiyo, nilimuagiza Katibu Mkuu ahakikishe kwamba wafanyakazi wote wenye madai mbali mbali awalipe fedha zao, hata kama kufanya hivyo tutakosa gharama za kuendeshea vipindi. *(Makofi)*

Naomba nimshukuru sana Katibu Mkuu agizo hilo alililiheshimu na malimbikizo yote ya wafanyakazi yamelipwa na hata watangazaji wetu hawa wanaochukua films hapa Barazani, basi bajeti zao za nyuma zimelipwa na hata katika Kikao hichi cha Bajeti fedha zao nyingi wameshalipwa na wanazo suti mpya nafikiria pia tumewapa suti moja moja, ili kuona waonekane vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Spika, matumizi ya haki za wafanyakazi yameongeza mori ya wafanyakazi na pia imesaidia kuongeza *moral* yao ya kazi. Kikosi cha Mafundi wa *ZBC* wa Unguja walisafiri na kwenda Pemba wakashirikina na mafundi wenzao wa Pemba na kuumiza vichwa vyao na kupanda juu ya mnara wa *Television* Kichunjuu wakiwa juu kwa masaa 10 *nonstop*. *(Makofi)*

Baada ya kuteremka Pemba nzima mpaka Gando na Kiwani *ZBC TV* inaonekana safi kabisa na hiyo ni *moral* yao na walisema hatuulizi posho wala *overtime* na wizara itatulipa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, matumizi haya ya kulipa malimbikizo ya wafanyakazi yametupunguzia uwezo wa kiutendaji kwa hivyo ni kweli sana, kwamba Masingini hivi sasa tunahitaji karibu shilingi 800,000/= hivi ili *generator* litu liweze kufanyakazi, yaani betri ya 120N yenye kugharimu shilingi 280,000/= pamoja na *service ya generator* lenye kubwa lenye kugharibu shilingi 500,000/= na hivi sasa fedha hizo hatuna.

Kwa kweli tunakwenda katika hali ngumu. Kwa mfano, juzi tulikopa *Air Condition* ya *Control Room* ya TV na jana pia tumekopa *Printer* kwa ajili ya *News Room* na tutaendelea kukopa pale ambapo tuhakikishe kwamba vipindi angalau vinakwenda. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tunaomba sana kwamba mapungufu yetu yasichukuliwe ndiyo hali tuliyonayo. Naahidi baada ya Baraza lako tukufu kupitisha bajeti yetu na Mhe. Waziri wa Fedha kufanya mambo yake mambo yatabadilika.

Mhe. Spika, kuhusu wafanyakazi waliokwenda masomoni mwaka 2003/2004 nchini Uholanzi na ambao hawakulipwa. Ni kweli kwamba hili suala lilifanyika huko nyuma, malipo yao hawajalipwa. Mimi mara baada ya kuona kwamba maslahi mengi ya wafanyakazi wanalipwa basi na wao walikuja kudai haki yao.
Ni kweli hii ni haki yao lakini bahati nzuri Mhe. Spika, kuanzia mwaka 1995 hadi mwaka wa 2010 mara tatu nilichaguliwa kuwa Mjumbe wa PAC, mara ya mwisho nilichaguliwa nikiwa pamoja na Mhe. Hija Hassan Hija na Mhe. Omar Ali Shehe. Sisi wakati tulipokuwa Wajumbe wa Kamati ya PAC tulikuwa wakali sana kwa Mawaziri waliokuwa wakiwaachia watendaji wao, wapuuze kanuni za matumizi ya fedha. Moja la muhimu sana kwa mujibu wa kanuni ya fedha ya mwaka 2006 kifungu cha 94.4 paragrafu 155 naomba ninukuu.

> *"For the purpose of finance of this finance regulation a payment voucher which is incomplete because of its supporting documents are missing voucher.*

Mhe. Hija Hassan hili analifahamu sana na mimi na yeye na Mhe. Omar Ali Shehe ilikuwa tunakaba sana Mawaziri kuona kwamba wanaruhusu watendaji wao walipe malipo ambayo hayana *supporting documents.*

Mimi Mhe. Spika, dai hili bila ya kuwa na *supporting document* ni vigumu. Ila naomba tupeane muda zaidi tuzitafute *documents* zenyewe ili nipate nafasi ya kuwalipa wafanyakazi hawa fedha zao. Kama hili haliwezekani basi ningeomba sana labda Mwenyekiti wa PAC kwa niaba ya Baraza lako tukufu akaniandikia barua ya agizo kwamba, pamoja na kwamba *supporting document* hizo hazipo, basi Waziri nakuagiza walipe. Nitatii agizo hilo la Mwenyekiti maana kamati baadae ikipewe taarifa yeye mwenyewe ndie atakaekuwa mas-ul.

Mhe. Mohamed Haji Khalid, namshukuru sana, maelekezo yake na ushauri wake waliotupa hasa kuhusu Shirika lisishindwa na Vyombo vya Habari binafsi. Hili naahidi kwamba nitalisimamia. Hili wazo nalichukua kama ni changamoto kwetu na pia maelekezo yake kuhusiana na michezo inayokwenda sambamba na mila, silka na utamaduni, tunayachukua na tunayafanyia kazi.
Mhe. Asaa Othman Hamad, namshukuru sana kwa mchango wake. Yeye ni Mjumbe wa Kamati ana jukumu kubwa kuona kwamba Wizara yetu hii inafanikiwa vizuri. Ushauri wake alioutoa kuhusu mnara wa Bungi nimeshaueleza. Kamisheni na Utalii pamoja na masuala ya michezo tumeyapokea na namuahidi kwamba tutayafanyia kazi. Rai yake kuhusiana na matumizi ya kiwanja cha Amani, kuhusu sherehe na gwaride tumelipokea tutakaa na serikali na kwa kweli serikali hili imeshaanza kulizungumza, lakini tutalizungumza zaidi kwa umakini mkubwa na tunashukuru kwamba Mhe. Assaa ametupa ushauri mzuri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub, naomba kumshukuru sana kama nilivyosema ni mwakilishi makini sana kwa wananchi wa Muyuni. Mara zote michango yake huwa mifupi lakini yenye kujenga na kuelekeza. Ushauri wake kuhusu waandishi wa ZBC kupelekwa Bungeni kwenda kuripoti vikao vya Bunge. Tunaufanyia kazi na tutashauriana kama yeye pia ni Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi.

Pia Mhe. Jaku Hashim, aliulizia gakwimu za mapato ya utalii. Kwa heshima kubwa namuomba Mhe. Jaku, ajue kuwa Kazi ya Kamisheni ya Utalii zaidi ni kusimamia sera ya utalii na kutangaza utalii wenyewe. Kazi ya kukusanya mapato yapo kwenye Bodi ya Mapato ya Zanzibar. Kwa hivyo namuomba akubali kusubiri jibu lake wakate wa bajeti ya Wizara inayosimamia Bodi ya Mapato hapa Zanzibar.
Pia alihoji kuhusiana na uwekezaji wa Hoteli ya Bwawani. Kimsingi hoteli ya Bwawani kunashughulikiwa na ZIPA ambapo tayari wapo wawekezaji wengi ambao bado wanawaangalia kwamba yupi atafaa kuwekeza.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir, namshukuru sana kwa mchango wake ametupa ushauri muhimu sana. Pia ametupongeza kuhusu mafanikio yanayonekana katika hoteli ya Bwawani. Naamini kwamba pongezi zake zitaleta mori zaidi kwa wafanyakazi wetu. Pia alitambua mafanikio ya *ZBC Radio* na Afisi ya Dar-es-Salaam, lakini akahoji mbona *ZBC TV* haionekani mafanikio yake.

Ni kweli Mhe. Spika, *ZBC TV* imechelewa kuanza kufaidika na Afisi yetu iliyokuwepo Dar-es-Salaam. Lakini matayarisho yamekamilika, mdhamini wa kipindi cha kwanza cha kuanza na matangazo ya magazeti kutoka Dar-es-Salaam ameshapatikana na hatua za majaribio zimeanza jana. Matumaini yangu kwamba si muda mrefu matangazo hayo yatakuwa hewani zaidi.

Mheshimiwa, alihoji kutoonekana kwa mtaalamu wa ishara. Ni kweli naomba niseme kwamba hata kwenye mashirika yaliyoendelea ya utangazaji wataalamu hawa wa ishara sio kwamba

wanakuwepo muda wote. Wao wanapangiwa kwa wakati maalum na kwa shughuli maalum. Sasa hivi sisi tulianza kwa majiribio na katika majaribio hayo tumegundua kwamba kuna umuhimu wa upatikanaji wa vifaa viwili ili kuepokwake kwa *ZBC TV* yetu uwe mzuri na uhakika zaidi. Vifaa hivyo tukijaaliwa vitanunuliwa baada ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kupitisha bajeti yetu.

Mhe. Hamza Hassan Juma, namshukuru sana na huyu ni mwenzangu wa siku nyingi, mchango wake umesaidia sana. Alitushauri kuangalia maslahi ya wafanyakazi wa Shirika hili. Naomba nimuahidi kwamba katika *scheme* hii ambayo itaandaaliwa, suala hilo litashughuki aidha mavazi na mambo mengine tutayashughulikia. Kuhusu suala la kukatika kwa matangazo ya jana kama ambavyo nilivyomjibu Mhe. Hija, naomba akubaliane na majibu hayo. Huo ndio ukweli wenyewe, lakini tutajitahidi kwamba matangazo yetu yawe yanapatikana saa zote .

Mimi binafsi Mhe. Spika, nilikwenda pale Masingini na Mhe. Naibu Waziri wa Makaazi na Umeme akiwa na kikosi chake cha mafundi kuangalia namna gani tutaweka umeme uwe *sustainable* kwa kweli wanafanya kazi vizuri.
Mhe. Hamza Hassan Juma, pia alizungumzia majaalia ya waandishi wa mawio na pia waandishi wengine waliokuwa hawajaajiriwa. Ukweli ni kwamba hawa ni waandishi wa aina ya *free lance* ambao malipo yao ni kwa kazi wanayoifanya. Ndio mtindo wa Mashirika ya habari mengi siku hizi wanakuwa na *free lance* wa aina mbili kuna wale wa 100% ambao wao wana haki ya kuuza huduma zao kwa mashirika mengine na *free lance* wa mkataba kama alivyo ndugu yetu Ali Saleh wa *BBC* yeye mkataba wake ni kwa *BBC* tu na hapa kwetu mashirika yetu ya habari yameanzisha utaratibu huu wa *free lance* 100% na pia *free lance* wa mkataba.

Kuhusu uwajiri utakaofanywa ni kamwa utaratibu wa Sheria ya Tume ya Uwajiri ni lazima kwanza nafasi itangazwe, pili pafanywe *interview* na atakaefaulu ndio ataajiriwa. Huo ndio muongozo wa Tume ya Utumishi hata hivyo inzari iliyotolewa na Mhe. Hamza Hassan naichukua na itafuatilia na niko tayari kushikiana nae katika kulisimamia hili.

Mhe. Spika, Mhe. Hamza pia na wawakilishi wengine walizungumzia suala la Mswada wa Baraza la Habari na haki ya kupata habari. Naomba niseme kwamba suala hili nilipewa nilipokuwa nikifanya ziara ya kutembelea Baraza la Habari la hapa tawi la Zanzibar. Nilimuagiza haraka Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo.

Katika kitabu chake cha Bajeti cha Wizara yangu ukurasa wa 30 paragrafu 35 kifungu kidogo cha 3 naomba ninukuu ili kuifanyia marekebisho Sheria Nam. 5 ya usajili wa magazeti na vijarida ya mwaka 1988. Mapendekezo yao yaliyotoa mwanga, tutayachukua, tutayaweka katika lugha ya kisheria, tutayarejesha tena kwa wadau wengine wote kabla ya kupeleka Serikalini na hatimaye katika Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, Mhe. Hamza Hassan Juma, pia alizungumzia wananchi wanaowadai wawekezaji Nungwi. Ningemuomba Mhe. Hamza mara baada ya shughuli hii kukamilika awaagize wananchi hao waje ofisini, niiagize Kamisheni ya Utalii iweze kuwasaidia. Kuhusu nyumba zinazogeuzwa gesti za *part time,* taarifa niliyonayo kwamba nyumba hizo hazijapewa leseni na Kamisheni ya Utalii. Hata hivyo Kamisheni ya Utalii watafuatilia kwa kushirikiana na vyombo vya Dola ili sheria iweze kuchukua mkondo wake.

Mhe. Hamza Hassan pia alizungumzia suala la Uwanja wa Amani naomba aridhike na majibu niliyoyatoa mbele ya Baraza hili kupitia hoja kama hiyo kwa Mhe. Nassor (Jazira). Na kuhusu mchango wake wa *Kick boxing* ambao pia Mhe. Jaku aliugusia. Naomba niseme kwamba hili ni suala nyeti. Muasisi wa mapinduzi yetu matukufu Mzee Abeid Amani Karume mara baada ya kufariki kulikuwa na maneno aliyoyasema hivi:

> "Kilichokuja na kuzikwa ni kiwiliwili chake tu, busara, fikra na mawazo yapo na yataendelea kudumishwa milele"

Busara ya Mzee wetu kupitia *standing order* yake ni kwamba boksing isichezwe Zanzibar. Unacheza kwa kanuni madhubuti yenye kuashirikia kumpiga mwenzio sehemu fulani na sehemu fulani usimpige. *Kick boxing* naambiwa ni mchezo wa mateke na magumi. Sasa ikiwa ni busara za baba yetu ametuelekeza kwamba ngumi tusicheze, akija akisikia huko akhera aliko tunacheza mateke na magumi kwa mpigo ndio kumuenzi au vipi.

Ushauri ambao naomba Mhe. Hamza Hassan aukubali ni kwamba ikishamaliza Ramadhani mimi na watu wangu wa Utamaduni na Michezo na yeye Mhe. Hamza na Mwenyekiti wa Kamati yangu ya Utalii na Mifugo, Michezo na Habari, tuje tujifungie katika *Gym* moja hapa Zanzibar, tualike timu moja ya *boxing* tuitizame halafu siku hiyo hiyo tualike timu nyengine ya *kick boxing* tutizame. Baada ya hapo tuzingatie na tutakayokubaliana tumpelekee Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa mazingatio yenye maslahi na wanamichezo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu, namshukuru sana kwa mchango wake mara nyingi michango yake huwa ni yenye miongozo muhimu na maelekezo yenye maana. Binafsi mimi namshukuru hasa pale anaponipa imani na moyo kwamba anategemea kwamba ufanisi unaweza kupatikana sana mbele ya Wizara hii ikiwa nitazidisha usimamizi. Hilo namuahidi kwamba nitalizidisha kwa umakini zaidi.

Mhe. Spika, ushauri wa Mhe. Ismail Jussa, kuisimamia zaidi *ZBC* nimeupokea zaidi na juu ya kuwasiliana na *BBC* juu ya mafunzo ya wafanyakazi wetu tutalizingatia na tutalisimamia hilo. Kuhusu Mkurugenzi Mkuu na Wakurugenzi wenzake kama hawaelewani nasikia jambo hili huko nyuma lilikuwepo lakini sasa limerekebishwa. Lakini hata hivyo Mhe. Jussa ni Mwakilishi wa Mjimkongwe na Karume House ipo Mjimkongwe, yumkini yeye amepata taarifa mimi sijapata. Ninachomuomba anipe nafasi nifatilie zaidi suala hili.

Kuhusu maendeleo na mapendekezo ya Baraza la Habari tumeyapokea na tumeanza kuyafanyia kazi kama nilivyosema katika Idara ya Habari Maelezo. Kuhusu wafanyakazi 10 wa kutwa walioahidiwa kuajiriwa. Nadhani hawa ni *free lance* kama nilivyoahidi kabla utaratibu wao ni huo na ikitokea nafasi ya ajira itabidi waingie katika ushindani kwa kufuata Sheria ya Utumishi wa Umma. Indhari ya Mhe. Jussa juu ya Kampuni ya *Star Times* tumeichukua nasi bado hatujakubaliana kuingia nao ubia.

Kuhusu suala lake la vipi Wizara imejipanga kutafuta *decoder* kwa kweli hili ni miongoni mwa sababu muhimu ya kutaka Shirika letu la serikali ndio awe *multiplex operator* ili iweze kumiliki uwezo wa kuwapatia wananchi *decoder* zenye ubora na bei nafuu.

Mhe. Spika, Mhe. Ismail Jussa alitushauri kuhusiana na kuwa makini viwango bora vya watalii na kutilia maanani kudhibiti mapato yanayo tokana na utalii. Ushauri tutaufanyia kazi, kuhusu

suala la Kanuni za Sheria za Utalii na ajira kwa Wazanzibari ninachoahidi ni kwamba nitamshikisha kila mdau katika kupendekeza kanunu madhubuti zitakazowafaidisha Wazanzibari wote. Hivyo ninakaribisha mapendekezo ya kanuni za sheria za Utalii katika Kifungu hicho cha Sheria, lengo ni utalii kwa wote.

Kwa hivyo, Mhe. Ismail Jussa akiwa yeye ni mwanasheria madhubuti ninamuomba msaada tusaidiane katika hili. Aidha suala la vinyago katika biashara ya utalii na mimi halinifurahishi hata kidogo. Lakini muhimu tuwe na mbadala wake. Ningetoa ushauri Wazanzibari wajiendeleze katika sanaa ya uchongaji na ufinyanzi ili watalii wanapokuja kwetu huhitaji zawadi ya kuchukua kwao itakuwa ni jambo la maana ikiwa vijana wetu wataibua ajira katika suala hili.

Bodi ya sanaa iko tayari ku shirikiana na vijana wetu katika kuendeleza vipaji vyao. Nimeambiwa Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale, kuanzia Oktoba mwaka huu, itapunguza asilimia 70 ya vinyago katika maeneo yake ya *Beit-el-Ajab* na kasri ya Mfalme. Pia Mhe. Jussa aligusia suala la matengenezo ya jengo la Kasri ni kweli hali yake inahitaji matengenezo haraka. Ninachomuahidi ni kwamba suala hilo tumelipeleka serikalini na tayari maamuzi yamefanywa kupitia bajeti hii, vyovyote iwavyo ili fedha ipatikane kutengenezwa nyumba ile yenye historia muhimu.

Mhe. Spika, kuhusu nyumba ya *Beit-el-Ajab* pale pana mradi wa *MACEMP* ndio waliopewa jukumu la matengenezo yake. Hata hivyo nitawasiliana kwa karibu na wasimamizi wa mradi huo ili kujua majaalia ya kazi ile.

Mhe. Spika, kuhusu vifungu mbali mbali ambavyo Mhe. Ismail Jussa, alivitaja wakati anachangia mchango wake. Ni kwamba kifungu cha Idara ya Utumishi Uwendeshaji kifungu 211101 Mishahara. Ongezeko la kifungu hiki linatokana na mabadiliko ya mishahara yaliyofanywa na serikali kuanzia Oktoba 2001. Aidha kifungu hichi kitatumika pia kwa ajili ya nyongeza ya mishahara na *promotion* kwa wafanyakazi wote wa Wizara. Nyongeza hizo zitaanza kutolewa kuanzia mwezi wa Julai kama Serikali ilivyoelekeza.

Mhe. Ismail Jussa, kuhusu kifungu cha Safari za Kikazi, kifungu hiki kimeongezeka kutokana na safari za kikazi hasa za Arusha, vikao vya *AAC*, Sherehe za kitaifa zote na ziara za ufatiliaji katika taasisi zilizoko Pemba, Dar-es-Salaam na maeneo mengine.

Mhe. Jussa, pia alizungumzia Idara ya Habari Maelezo 220400 cha Mafuta cha shilingi 14 milioni, akipiga hesabu chap chap atagundua kwamba zile ni karibu kama lita 500 kwa mwezi. Kwa Idara nzima ya Habari Maelezo nafikiria lita 500 ni *reasonable* sana, ukitilia maanani kwamba wana shughuli mbali mbali, wanagari la snema, wanashughuli hizi na hizi. Nahisi kwa lita 500 kwa mwezi ni kiwango cha mafuta ambacho hakina tatizo.
Kuhusu suala la kifungu cha Kamisheni ya Utalii kifungu 21101 Malipo baada ya saa za kazi, bajeti iliyopita ilikuwa ni shilingi milioni kumi na laki nane, mara hii imeongezeka kufika shilingi milioni 40. Ongezeko hili limetokana na ongezeko la mishahara kuwalipa *Tourism Patrol Unit* ambayo idadi yao na harakati zake zitakuwa zimezidi, Maafisa wa Habari Bandarini Uwanja wa Ndege, Bwawani Kituo Kipya cha Kutoa Habari kinategemewa kufunguliwa Ngomekongwe.

Kifungu 2116 Posho Vikao na Kamati bajeti iliyopita ilikuwa milioni 30 lakini bajeti hii ni milioni sitini na mbili milioni, laki moja ishirini na saba. Kifungu hiki kabla yake kikitumika kwa ajili ya Wajumbe wa Bodi ya Kamisheni ya Utalii iliyokuwepo. Bodi hiyo ilikuwa na mwenyekiti na wajumbe watano na katibu. Baada ya marekebisho ya Sheria ya Utalii Nambari 7 ya mwaka huu kifungu Nambari 5 kimeonesha kuwepo kwa Mwenyekiti, Makamishna wanane na Katibu Mtendaji.

Aidha Kifungu 11(a) (i) kimeanisha kuwepo kwa vikao viwili kwa mwaka vya Wadau wa Utalii, (*Tourism Stop Order Forum)*. Kifungu 23(a) (i) kimeainisha uwanzishwaji wa Kamati za Utalii za Wilaya, kila Kamati itakuwa na wajumbe 13 katika kutekeleza dhana ya Utalii kwa wote, Kamisheni itawajibika kufanya semina Mikoani, Wilayani, Shihiya na kwa viongozi mbali mbali.

Kifungu 220203 na 22021 Chakula Vinywaji na Viburudishaji, bajeti ya mwaka jana vilikuwa na shilingi milioni tano laki tano, lakini bajeti ya mwaka huu zimeongezeka hadi kufika shilingi milioni thalathini, laki mbili sabini na mbili elfu. Ongezeko hili limetokana na kuongezeka vikao kama nilivyoainisha hapo hapo juu. Kamati za Wilaya kwa kweli zitakuwa na shughuli nyingi.
Mhe. Ismail Jussa Ladhu, alihoji kifungu cha 263173 Uimarishaji wa Utalii na bajeti ya mwaka huu imeongezeka hadi shilingi sabini na tisa milioni laki tatu sitini na moja. Kifungu hiki kinatumika kwa:

- Kuchapisha kalenda za ukutani, majarida ya utangazaji ya lugha mbali mbali,
- DVD,
- Matangazo katika majira ya Kitaifa na Kimataifa,
- Kulipia ada ya Ushirika wa Maonyesho,
- Kukidhi mahitaji ya Waandishi wa Habari wa nje wanaoalikwa na Mheshimiwa.

Mhe. Spika, pia Mhe. Ismail Jussa Ladhu, alihoji kifungu 211101 Posho maalum. Kifungu hiki kimezidi kutokana na Kamisheni kulipa mishahara ya Kamishna, Makatibu Watendaji wawili, dereva na matarishi watatu.

Kifungu 220710 fungu hili limekusanya fedha kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa uwanja wa Amani na fedha kwa ajili ya matengenezo ya nyumba ya sanaa iliyopo Mwanakwerekwe.
Kifungu 282118 kifungu hichi kinatumika kusaidia timu za Taifa na Vilabu vinavyoshiriki mashindano ya kimataifa.

Mhe. Spika, nadhani hayo ndiyo mambo mengi Mhe. Ismail Jussa Ladhu alihitaji katika vifungu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, alizungumzia mambo mengi. Naomba kwanza nimshukuru kwa mchango wake. Hakika mchango wake unatuweka sisi na watendaji wetu tuwe makini zaidi. Naomba aridhike kuhusiana na majibu niliyotoa kuhusiana na Shirika la Utalii na wafanyakazi wa Bwawani kuhusu namna inayowasaidia wahitimu wake kupata ajira. Kwanza chuo kinajitahidi kutoa taaluma yenye kiwango na pili chuo kimejenga uhusiano na wenye mahoteli ili wanafunzi wake waweze kufanya mazoezi kwa vitendo.

Hilo linasaidia kuwapa wanafunzi wetu kujiamini na pia kuyazoea mahoteli makubwa. Hivi karibuni hoteli na Briiz ilioko, Bwejuu iliajiri vijana wetu saba kupitia chuo.

Mhe. Spika, Mhe. Mbarouk Wadi Mussa pia alizungumzia Kampuni iliyochukua umeme kutoka kituo cha *ZBC* Masingini. Kwanza sio sahihi kwamba Kamati yake ya *PAC* ndiyo iliyotoa amri umeme huo uondolewe. Ukweli ni kwamba katika ziara yangu ya kukagua sehemu ya kazi baada ya kupewa damana hii nilipofika Masingini niligundua kwamba kuna waya umetoka kutoka kituo cha Masingini kuingia kwenye Afisi ya mtu binafsi. Nilipouliza nikaambiwa waya huo umeungwa miaka mingi kwa makubaliano baina ya Shirika la *ZBC* na Kampuni hiyo ya Zanlink kwamba Idara ya *TVZ* wakati huo watowe umeme na wao Idara ya *TVZ* wapate mawasiliano ya *Internet* bure kwenye mitambo yao ya Karume House.

Mimi hapo hapo nikaamrisha chini ya usimamizi wa Katibu Mkuu makubaliano hayo yavunjike na nikawapa siku moja wahakikishe kwamba waya huo wa umeme umekatwa. Kwa kweli suala hili lilitekelezwa. Namshukuru na Mwenyekiti, wa *PAC* alipotembelea. Yeye alinipongeza kwa hatua hiyo niyoichukua. Alinipigia simu akanambia Mheshimiwa tumeona jambo zuri umelifanya na tunakupongeza kwa hatua hiyo. Naomba Mhe. Mtando ajue kwamba shughuli hii sisi tumeshawahi kuifanya.

Pia Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) alizungumzia suala la kuhamishwa kwa Shirika la Magazeti kutoka jumba la zamani la Redio kwenda jumba jipya la Redio. Mhe. Spika, zote mbili Shirika la *ZBC* Radio na Shirika la Magazeti ni taasisi zilizochini ya Wizara yangu. La msingi ni kwamba Shirika la Magazeti la Serikali halijawa na jengo lake la kudumu. Uamuzi wa kulitumia jengo lile la radio la zamani lilichukuliwa karibu miezi sita iliyopita la uongozi wa Shirika la gazeti uliarifiwa. Mimi nilipotembelea pale katika kujitambulisha uongozi wa Shirika ulinilalamikia kuhusiana na suala hili. Kimsingi serikali iliamua kulitumia jengo lile la zamani la redio ambalo lilikuwa na studio kubwa ya kurikodiya zamani, lirejeshe matumizi yake ya kihistoria, litengenezwe, liwe jengo la kisasa la kurikodia muziki na sanaa ikiwa ni ahadi ya Mhe. Rais wa Zanzibar Dokta Ali Mohammed Sheni katika kampeni zake za uchaguzi.

Uongozi wa gazeti ulipewa taarifa ya kuhama rasmi tokea tarehe 14 mwezi wa 6 na ilipofika tarehe 7 mwezi wa 7 karibu wiki tatu walihama. Aidha hata Makamo Mwenyekiti wa Bodi ya Shirila la Magazeti ya Serikali ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha ya Baraza lako tukufu Mhe. Salmin Awadh Salmin naye alililalamikia katika hili tukafuata pamoja mimi na yeye, mguu kwa mguu, tukenda katika majengo yale. Nafurahi kwamba aliridhika na eneo ambalo shirika lake amepewa nafasi.

Mhe. Spika, la msingi kwa niaba ya Wizara nakubali kwamba ni wakati sasa Shirika la Magazeti liwe na majengo yake ya kudumu na naahidi kwamba nitashirikiana na bodi hasa Mwenyekiti na Makamo Mwenyekiti ni watu wangu wote wa karibu kabisa kuona kwamba tatizo hili limeondoka. Kuhusu vifungu vya matumizi mbali mbali ambavyo Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando), alivitaja kuona kwamba tatizo hili limeondoka.

Kuhusu vifungu vya matumizi mbali mbali ambavyo Mhe. Mtando alivitaja na alihoji vifungu vingi na nitajitahidi kwa wakati wako uliobaki nitajitahidi kumjibu vifungu vyake.

Alisema kifungu cha viburudishaji, kifungu hichi kinatumika kwa ajili ya vikao vya Wizara kila siku ya Jumatatu. Lakini pia Idara ya Utumishi na Uendeshaji inaofisi 5,

1) Ofisi ya Waziri,

2) Ofisi ya Naibu Waziri,

3) Afisi ya Katibu Mkuu,

4) Afisi ya Naibu Katibu Mkuu,

5) Afisi ya Mkurugenzi.

Mhe. Spika, ofisi hizi tano tunapokea wangeni mara kwa mara na haiwezekani aje mgeni umtizame macho. Sisi tukenda kwa watu tunakirimiwa sisi tuwaangalie macho. Hilo haliwezekani Mheshimiwa. Kwa hivyo ofisi hizi tano pamoja na vikaa mbali mbali, Mheshimiwa hizi pesa sio nyingi sana. Naomba Mhe. Mtando akubali na naamini kwamba yeye ni sahibu wangu mkubwa sana na atakubali kwa hilo.

Mhe. Mtando, aliahidi suala la *fumigation*. Ni kweli kwamba tumetenga fedha kwa ajili ya fumigation, tuna shughuli mbali mbali tunazifanya. Jengo lile tulilonalo Mhe. Spika, wewe ndio ulieliwacha sasa lina mambo mengi. Lakini tutajitahidi kuona kwamba tunalishughulikia ili liweze kukalika vizuri na wafanyakazi wetu.

Pia Mhe. Mtando alitaja kifungu cha 22051 vifaa vya michezo, pamoja na maandalizi na ununuzi wa vifaa vya timu za mpira wa miguu na mpira wa Wizara. Mwaka jana ilichukua ushindi na mwaka huu tunajitapa kushiriki mashindano mbali mbali sio haya tu lakini na mashindano mengine pia.

Mhe. Mtando pia alihoji kifungu 220701 matengenezo madogo ya ofisi. Kifungu hiki ni kwa ajili ya matengenezo madogo madogo ya ofisi pamoja na ukarabati wa Ukumbi wa juu wa mikutano ya Wizara. Ukumbi mdogo wa mikutano kule juu tuishukuru sana Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ametupa tena sisi kuwa zoni zetu na unahitaji matengenezo makubwa. Kwa hiyo tuna mambo ya kulifanyia shughuli hiyo, kwa hivyo Mhe. Mtando akubali na hilo.

Kuhusu kifungu 220702 matengenezo makubwa ya jengo, kifungu hiki ni kwa ajili ya matengenezo makubwa ya jengo la Rahaleo kama nilivyosema kuligeuza kuwa studio ya kisasa ya kurikodia muziki. Hii ni ahadi ya Mhe. Rais wa Zanzibar ambaye mara nyingi amekuwa anaitoa. Bajeti ya mwaka jana mradi huu uliingiziwa shilingi 125 katika fedha za *development* ambazo ndizo zimeanza kutumika. Mwaka huu fedha kupitia *development* hazikupatikana na hivyo Wizara tumeamua kujikamua ili kupata fedha kwa ajili ya kutimiza ahadi ya Mhe. Rais. Hatuoni raha kwamba ifike labda mwaka mmoja kabla ya uchaguzi ndio tuanze kukurupuka kutimiza ahadi ya Mhe. Rais, itakuwa hatukumfanyia jambo la maana hata kidogo. Naomba Mhe. Mtando alikubali hilo.

Kwanza naomba afahamu kwamba wizara yetu ni Wizara inayoshughulikia mambo mengi ya mawasiliano. Kwa hivyo bado inahitaji vifaa vingi vya kompyuta. Kwa utaratibu wa kisasa masuala ya *type writer* zile zimepitwa na wakati. Ni lazima watendaji, wafanyakazi mbali mbali

wawe na kompyuta. Naamini na yeye Mhe. Mtando anayo kompyuta kwa hivyo hili ni jambo la kulishughulikia vizuri sana.

Mhe. Mtando pia alihoji kifungu 221101 Mafunzo. Kifungu hiki kimeongezeka kutokana na wafanyakazi 13 ambao watakuwa katika mafunzo ya muda mrefu. Tumekubaliana Serikalini kwamba kila Wizara ijitahidi kusomesha watu wake. Sisi kama nilivyosema nilivyokuwa nikijibu hoja za ZBC tunamahitaji makubwa ya wataalamu kwa hivyo kisingepanda kwa kifungu hicho ni kwa sababu hiyo.

Mhe. Mtando alihoji pia kifungu cha ushauri nasaha. Mhe. Spika, Kifungu 223178 Ushauri Nasaha, naomba Mheshimiwa akubali kwamba shughuli hii ni muhimu, inahitaji kusimamiwa vizuri ili kuona janga hili limetokomezwa. Pia alihoji Kifungu cha 2211202, ununuzi wa sare, anataka maelezo.

Mheshimiwa shilingi milioni moja la laki tano, kwa wafanyakazi kwa kweli hii ni pesa ndogo sana, kwa ununuzi wa sare kwa wafanyakazi mbali mbali, madereva, matarishi, walinzi. Mhe. Mtando tukubaliane hili kwamba lipo katika *reasonable*. Pia alihoji shilingi milioni mia nane, kifungu 220517, Idara ya Mipango Sera na Utafiti. Fedha hizi zilitengwa hapa kwa ajili ya kazi zifuatazo:

- Utayarisha vitabu vya muelekeo wa mpango wa kazi,

- Kutayarisha vitabu vya MTEF na Bajeti ya Wizara ya mwakani,

- Kutayarisha vitabu vya utekelezaji wa miezi mitatu kwa Kamati ya Mifugo, Uvuvi, Uwezeshaji na Habari, pia maeneo mengine mbali mbali ya utayarishaji wa matengenezo.

Mhe. Mtando pia aliyoji kifungu 220701 Afisi Kuu Pemba shilingi 67 milioni. Shughuli hii ni ununuzi wa bati kwa matengenezo ya paa Afisi Kuu Pemba, ununuzi wa mbao, ununuzi wa madirisha ya *aluminium*, ununuzi wa *flow tails* kwa ajili ya Afisi kuu Pemba. Ununuzi wa milango mikubwa Afisi Kuu na gharama za ujenzi wa malipo kwa mafundi.

Mhe. Mtando pia alihoja kifungu cha Idara ya Makumbusho 220701, matengenezo ya majengo Unguja, fedha hizi zitatumika kwa ajili ya majengo 10. Sasa shilingi milioni nane laki mbili Mhe. Spika, kwa majengo kumi kwa kweli nafikiri Mhe. Mtando atakubaliana nayo. Pia matengenezo kama hayo 220701 milioni 7 kwa ajili ya matengenezo Pemba, fedha hizo zitatumika kwa ajili ya matengenezo saba ya kihistoria kama ilivyoainishwa katika malengo makuu.

Mhe. Mtando pia alihoji kifungu cha 31201 fedha hii itatumika kwa ajili ya ununuzi wa vespa, kwani mwaka uliopita walishindwa kununua fedha hizi, milioni mbili na laki tano zitatumika kwa ajili hiyo. Kifungu nambari, 211, posho maalum. Fedha hizi zitatumika kwa ajili ya maposho ya Mkurugenzi, Sekretari, Mwanasheria, tarishi, dereva wa masjala.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia kama nilivyosema awali, nishukuru sana michango ya Mhe. Shadiya kwa kweli nimshukuru amenishauri vizuri, naomba nimuahidi kwamba yale yote aliyozungumza nitayafanyia kazi.

Mhe. Farida na yeye namshukuru kwa mchango wake amenipa moyo, amenielekeza na kunishauri vizuri naahidi kwamba ushauri wake pia nao utafanyiwa kazi. Aidha pia namshukuru sana Mhe. Ali Mohammed wa jimbo la Mkoani kwa ushauri wake na maelekezo yake katika kuona kwamba Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo pia silka za mila nyengine pia zinapata nafasi ya kuendelea.

Mhe. Spika, kama nilivyoanza kusema kwamba niendelee kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa michango yao ya ushauri wao. Kwa kweli michango yao mbali mbali waliyoitoa jana wamenisaidia sana Mhe. Spika, na imekuwa ni chachu kwangu na itanisaidia sana. Nimejitahidi sana kwa kadiri ya uwezo wangu kuwahoji wahehimiwa wajumbe katika kukidhi mahitaji ya hoja zao. Inawezekana kwamba pale na hapa labda nimesahau na sikufanya hivyo kwa dharau lakini kwa sababu ya mambo mengi yaliyoulizwa lakini pia kuangalia leo ni Ijumaa siku adhimu ya kwenda Msikitini.

Mhe. Spika, niendelee tena kuwashukuru wafanyakazi wa Wizara yangu kwa kunisaidia sana na hasa Naibu Waziri na watendaji wengine, vyombo vya habari mbali mbali vimenisaidia sana vya Serikali binafsi kama Zanzibar Cable inajitahidi sana na naipongeza sana na redio nyengine binafsi. Baada ya hayo Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri, wanyanyue mikono. Wanaokubali, wanaokataaa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza lako limejadili na kukubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Habari Utamaduni Utalii na Michezo, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama kamati ya matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 31 – KAMISHENI YA UTALII

Kifungu 0201 Utawala Unguja

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ninashukuru Mhe. Mwenyekiti na kwa sababu ndio wa mwanzo kusimama katika vifungu naomba kwanza nimshukuru na nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wake wa kina wa maeneo mengi ambayo tumeyachangia.

Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nilizungumzia suala la mapato yanayotokana na sekta ya utalii na ninashukuru Mhe. Waziri katika majibu yake kanambia kwamba mawazo yetu atayafanyia kazi lakini nilikuwa naomba zaidi ya jibu hili la jumla kwamba mawazo yetu yanachukuliwa. Kwa sababu suala hili la mapato linatokana na sekta ya utalii bado limekuwa ni

tatizo kubwa sana na mara nyingi serikali imekuwa ikiahidi kwamba italifanyia kazi. Kuna maeneo mbali mbali tuliyoyataja kwa mfano katika masuala ya visa unapoingia hapa, masuala ya namna mihuri inagongwa pale airport na masuala mengine kama hayo. Tunaomba hebu Mhe. Waziri atusaidie kwamba kajipanga vipi katika kufanyia kazi hayo mawazo yetu tunampa kwa sababu waliopita wengi wametuahidi kwamba yanafanyiwa kazi lakini bado suala hili linaendelea kutusumbua.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti ni kweli kwamba Mhe. Jussa alizungumzia suala hili la mapato na nilimwambia kwamba suala hili tumelichukua na tunalifanyia kazi na ni kweli tumeanza kulifanyia kazi kwa sababu maeneo ambayo shughuli hizi zinafanyika ni mbili hasa. Moja ni pale bandarini na uwanja wa ndege. Pale bandarini tumeshakubaliana na Idara ya Uhamiaji kwamba sasa wafanyakazi wa Kamisheni ya Utalii watakuwa ndio wa kwanza wao wakija watalii zile fomu za kujaza kama wageni au vipi huwa zinapita pale kwanza kabla ya kwenda pale Uhamiaji. Sasa katika hali hii tumeweza sasa kujua wageni wanaokuja na kudhibiti mapato yetu.

Lakini suala lipo katika uwanja wa ndege wa Zanzibar, jambo hili tunalifanyia kazi kwa sababu tatizo liliopo ni kwamba nafasi pale ni ndogo, kuingiza pale mtu wa Kamisheni ya Utalii na mtu wa Uhamiaji ni jambo ambalo kidogo ni gumu kutokana na mazingira ya pale. Sasa watu wangu wa Kamisheni ya Utalii wanajaribu kuweka jicho lao vizuri, lakini tumekubaliana na Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu kwamba utapofunguliwa uwanja mpya basi tupewe chumba kikubwa ambacho watu wa Kamisheni ya Utalii na watu wa Uhamiaji watakuwa pamoja. Kwa hivyo yale mambo ya visa na mambo mengine mtu wetu wa Kamisheni atakuwa tayari anaona ili kujua kwamba hali hiyo inafanyiwa kazi. Kwa hivyo sikumwambia kwa bahati mbaya lakini kuna mikakati ambayo tayari tumeshaifanyia kazi na tumeshakubaliana serikalini.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti ninamshukuru kwa maelezo yake na nakubali kwamba kunaonekana umakini katika kulifatilia tofauti na yale majibu ya jumla jumla tu. Mimi ningeomba kutoa pendekezo moja halafu Mheshimiwa tuendelee, kwamba kama alivyosema mwenyewe bandarini wamejitahidi lakini atakubaliana na mimi Mhe. Waziri kwamba pahala ambapo tunaingiza watalii wengi zaidi ni uwanja wa ndege kuliko bandarini ndio mlango ambao wengi wanaingilia. Na Mheshimiwa hapo ndipo haya malalamiko mengi yapo, lakini kama vile vile kama nilivyosema suala hili linajumuisha taasisi nyingi. Iko tuhuma kwamba wakuu wa Idara ya Uhamiaji hapa Zanzibar wana mchezo wao katika haya lakini pia na wengine.

Sasa mimi nilikuwa naomba kwamba wakati ninalifanyia kazi hili la kungoja mpaka terminal mpya ambayo tunajua matatizo yake na hatujui litamalizika lini kutokana na mzozo ambao upo pale. Nilikuwa naomba hili katika mazingira haya ya sasa watafute utaratibu ambao sijui kwa kuweka Ofisa wa Kamisheni ya Utalii ama katika kushirikiana na Idara ya Uhamiaji kama kuna visa maalum badala ya kuwa kuna mhuri tu. Kwa sababu wa wenzetu tumezoea hata visa inayotolewa airport huwa mara nyengine huwa kama mfano wa stiker maalum zinazojulikana zina mhuri maalum si rahisi kughushiwa zile unabandikiwa katika paspoti yako pale pale unaingia tumeyaona hayo Mhe. Mwenyekiti tunaposafiri.

Kwa hivyo hili naomba walifanyie kazi kwa pamoja kwa sababu naamini kuna mapato mengi sana ambayo yanavuja pale, kwa sababu kuna watendaji na pengine wakuu wa Idara kama ya

Uhamiaji ambao wanashirikiana nao katika kuhakikisha ndio maana Mhe. Mwenyekiti utakuta mara nyengine wakuu wa Idara hii ya Uhamiaji imekuwa kama hii ndio milki yao katika kupanga watu maalum, kwa sababu wanapanga watu ambao watakwenda kufanya nao kazi katika suala la kukusanya mapato hayo. Kwa hivyo nilikuwa naomba Mhe. Waziri alitazame kwa makini ninamuamini sana Mhe. Said Mbarouk Nimena kazi aliyoifanya kwa kipindi kifupi lakini ninampa changamoto kwamba hili alifanyie kazi kwa karibu na serikali kwa ujumla mapato yetu katika sekta mama sasa hivi yanayoingiza mapato ya utalii yasipotee. Naomba sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti ushauri wake tutaufanyia kazi kama nilivyomuahidi na tutashauriana na Mhe. Waziri wa Nchi, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo, ambayo masuala ya mapato naye mkali kweli kweli, kwa hivyo tutapata uzoefu kutoka kwake tufanye kazi.

Kifungu 0201	Utawala Unguja	1,202,000,000
Jumla ya Fungu		**1,202,000,000**

(Kifungu kilchotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Marekebisho fungu 42 Wizara ya Habari Utamaduni Utalii na Michezo, Makadirio ya Mapato yakayokusanywa kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, jumla ya shilingi 556,200,000 Wizara ya Habari Utamaduni Utalii na Michezo. Vifungu vya fungu hili vinavyooneshwa hapa chini mapato yake yatasimamiwa na Katibu Mkuu Wizara ya Habari Utamaduni Utalii na Michezo.

Kifungu 0701	Idara ya Habari Maelezo	15,500,000/=
Kifungu 0702	Tume ya Utangazaji	

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha Ijumaa ya leo tukiwa wazima kabisa wenye afya njema na tunamuomba Mwenyezi Mungu atuepushe na kila shari zote.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kwanza nimpongeze sana mjumbe wangu wa zamani wa kamati ya Fedha na Uchumi ambaye sasa hivi amekuwa Waziri mimi niko back bancher. Mhe. Mwenyekiti kazi aliyoifanya ndani ya miezi mitatu kwa kweli tunaridhika nayo na hivi sasa mimi sitaki wengine waone choyo lakini bora tuseme wengine waone choyo wajitahidi.

Mhe. Omar Yussuf Mzee tunamshukuru sana kwa sababu hii changamoto yote anayotupa kutafuta vifungu fedha ziko wapi tunasimamia yale majukumu aliyotupa na tunayatekeleza. Kwa hivyo katika waziri makini Mhe. Omar Yussuf, lakini Mhe. Haroun Ali Suleiman Mheshimiwa katika mawaziri wanaofatilia maelekezo yetu tunamshukuru sana. Sasa hivi tumepata na mwengine wa tatu Mhe. Said Ali Mbarouk tunakupongeza tunakuomba uendelee.

Ninakuja katika hoja, Mhe. Mwenyekiti nilipokuwa nikichangia nilieleza katika hii Tume ya Utangazaji na nilieleza kwamba kuna malipo ambayo yanayotoza kuna baadhi wanatoza katika

interms of dollar. Sasa nilikuwa nataka nijue utaratibu unakubalika katika kusajili hizi taasisi zinazohusiana na broadcasting kukusanya fedha kwa dola nilikuwa nataka ufafanuzi kwa hilo, halafu baadae nikishapata majibu yaliyokuwa mazuri tutaendelea.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mawaziri musiwe na wasiwasi maana *assessment* za Mwenyekiti pale msije mkauliza sasa mie sijui niko wapi, ni mtazamo wake tu kwamba kuwafanya wengine kama hawajajitahidi wajitahidi zaidi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti ni kweli kwamba Mhe. Mwenyekiti wangu wa zamani alipokuwa anachangia katika bajeti yangu alihoji suala la ulipwaji wa dola. Mheshimiwa kwa kweli nimejaribu sana kuangalia sheria ya fedha ya mwaka 2005 na kanuni yake, lakini hilo sikuliona kama linakataza. Ninayo hapa nimekuja nayo makusudi kwa sababu hoja za Mhe. Mwenyekiti mimi huwa ninazipa thamani kubwa kwa hivyo nimekuja nayo hii. Jana usiku nilikipitia sana hiki kitabu kuona kwamba kanuni zetu za fedha zinakataza, bahati mbaya sikuona. Sasa nilipokuwa sikuona nikaona kwamba mwanasheria anatwambia kitu kama hakikutazwa katika sheria basi kufanywa si vibaya. Kwa hivyo sijapata maelekezo mengine kama suala hili haliruhusiki kisheria.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti ndio maana nikasema tunamshukuru sana Mhe. Said kwa sababu alikesha kwa ajili ya masuala yetu. Sasa nilikuwa tu naomba ajaribu kukaa na hawa watu wake wa hii Tume ya Utangazaji ili kujaribu kuliangalia hili, pamoja na kwamba sheria yetu ya fedha haikuangalia, lakini unajua dola kila siku inakuwa inapanda thamani. Sasa ajaribu kuangalia kama itakuwa inawaumiza kidogo hawa kwa sababu hawa wanatusaidia kuleta ajira, hawa ambao wanaoanzisha vyombo vya habari. Sasa tunaomba kwamba tusiwabane sana ili wengine wakaja wakaona labda masharti yetu magumu. Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti kwa kuwa Mheshimiwa kaahidi atalifuatilia, naomba tuendelee.

Kifungu 0702	Tume ya Utangazaji	33,000,000
Kifungu 0704	Shirika la Utangazaji Zanzibar Unguja	

Mhe. Ashura Shariff Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti wakati nilipokuwa nikichangia nilizungumza juu ya hili Shirika la Utangazaji. Mhe. Waziri alinipatia majibu lakini kwa kweli hayakunitosheleza, kwani nilizungumza kadhia ya wafanyakazi waliofukuzwa katika shirika hili. Kwa hivyo Mhe. Waziri ninamuomba ufafanuzi wa kina ili nimuelewe. Kwa sababu wafanyakazi hawa wamesimamishwa kazi, lakini hawakupatiwa hata barua. Na kwa bahati wameshaajiriwa wengine wapya kwa muda huu mfupi. Hebu aniambie ni sababu zipi mishahara yao hawa itapatikana vipi kwa muda wa wiki moja tayari wengine wapya wameshapata ajira hapa. Kwa hivyo anieleze vizuri na hawa ambao tayari wameshasimamishwa bila kupatiwa barua, je ni utaratibu huo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti ninakushukuru na ninamshukuru sana Mhe. Ashura kweli kwamba alizungumza suala hili na kama ambavyo alidai jana na mimi nilifatilia na katika kufuatilia nilimpigia simu mmoja anaitwa Mwanakhamis Juma nambari yake ya simu 0777 462357 nikamuuliza Bi Mwanakhamis uko wapi akanambia niko nyumbani, unafanyakazi wapi akanambia *ZBC* ati umesimamishwa kazi anambia la hasha

nimehamishwa tu sehemu yangu ya kazi kwa bado huyu ni mfanyakazi na mshahara wake utakuwa upo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ashura Shariff Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa vile Mhe. Waziri anasema kwamba bado hajasimamisha kazi, lakini taarifa niliyoipata mimi ikiwa sahihi ikitoka huko kabisa ni kwamba wamesimamishwa kazi bila ya kupewa barua. Lakini kwa sababu Mhe. Waziri anakiri bado ni wafanyakazi nakubali fungu hilo lipite.

Kifungu 0704	Shirika la Utangazaji Zanzibar Unguja	280,700,000
Kifungu 1001	Idara ya Utamaduni	17,000,000
Kifungu 1101	Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale Unguja	210,000,000
Jumla ya Fungu		**556.200, 000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati Bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu nambari 31 Kamisheni ya Utalii, makadirio ya fedha zinazohitajika kwa mwaka unaoishi tarehe 30 Juni, 2013 kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo ni jumla ya shilingi 1,318,000,000 Kamisheni ya Utalii. Vifungu vya fungu hili vinavyooneshwa hapa chini matumizi yake yatasimamiwa na Mkurugenzi Mkuu Kamisheni ya Utalii.

Kifungu 0201

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwanza naomba nianze kwa kumshukuru Mhe. Waziri kwamba vifungu vingi ambavyo nimetaka maelezo amenipa na nimeridhika na maelezo yake katika Kamisheni hii ya Utalii lakini inawezekana kwa tulitaka maelezo ya vifungu vingi vyengine kidogo, tulimpita lakini nina hakika atakuwa na nyaraka zote atatusaidia pale. Mhe. Mwenyekiti sina hoja tena kuhusu suala la posho za vikao kalifafanua kutokana na marekebisho ya sheria tuliofanya, la viburudishaji kalilifafanua bado nilikuwa naomba maelezo kwake kwamba fungu lile la mwanzo la mishahara ya fedha taslim kuna fungu la malipo baada ya saa za kazi ambalo limeongezeka sana hili hakuligusa, nilikuwa pia naomba maelezo niliomba kwamba kuna milioni arubaini pale ukilinganisha na ilivyokuwa. Lakini vile vile nimeomba maelezo katika fungu la safari katika Kamisheni ya Utalii ambalo pia nimesema limeongezeka sana kutoka mia moja sabiina na tisa milioni laki saba thalathini elfu mwaka jana hadi mia tatu na tisa milioni, laki moja arubaini na mbili elfu hilo Mhe. Mwenyekiti unalipat ukurasa 494 juu pale.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti nilitaka maelezo ya fungu la uimarishaji utalii na akatoa maelezo yake. Hapa nina angalizo tu Mhe. Mwenyekiti, kanieleza kwamba wanachapisha majarida, wanachapisha kalenda hapa ninamuomba Mhe. Waziri na pia Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo waangalie sana Mhe. Mwenyekiti kama kuna maeneo na hili ninalizungumza nina uzoefu nalo, bahati nzuri na masahiba zangu wa karibu amba wanafanya kazi za uchapishaji katika maeneo ambayo watendaji wengi huwa wanashirikiana na wachapishaji waliokuwa si waaminifu ku-inflet figure za gharama za uchapaji

na kuitia hasara mara nyingi serikali fedha kuingia mifukoni mwao kuliko kutumika kwa shughuli iliyokusudiwa, basi moja katika gharama hizi za promotion. Kwa hivyo nilikuwa naomba hili Mheshimiwa nakubali liendelee lakini nilikuwa ninamuomba Mhe. Waziri hili ajiridhishe sana juu ya zile *costing* hasa za masuala ya *promotion*.

Lakini kama nilivyosema Mhe. Mwenyekiti naomba maelezo katika yale ambayo hajayatolea maelezo ambalo ni fungu la posho la malipo baada ya saa za kazi ambayo imeongezeka sana na lile la safari za nje ambalo pia limeongezeka sana. Naomba maelezo katika hayo Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti ninakushukuru na ninamshukuru Mhe. Jussa kwa concern yake. Mheshimiwa Kifungu cha 21107 malipo baada ya saa za kazi ni kweli kimeongezeka kutoka milioni kumi laki nane mpaka milini arubaini. Mhe. Mwenyekiti jana Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dr. Mwinyihaji nilikwenda kuzindua kikosi kinaitwa *Tourism Patrol Unit*, nilikuwa na *passing out* hapo jana akenda kufanya hii kazi. Sasa hawa ni watu ambao kwa kweli Mhe. Mwenyekiti watakuwa na kazi moja kubwa kuhakikisha kwamba utalii wetu umekuwa salama. Tumekuwa na matatizo mengi ya karibuni ya watalii kuvamiwa mahoteli kuvamiwa. Kwa kweli imetuletea taswira mbaya huko nje ya nchi.

Serikali imeamua kuanzisha kikosi hichi na katika kufanya kazi hizi lazima kutakuwa na expenses ambazo *we have to anchor* sasa moja ni malipo baada ya saa za kazi. Kwa hivyo tumeziweka pale si lazima tuzitumie zote lakini tujiweke vizuri kuona kwamba vijana hawa wasije kuvunjika moyo baada ya kuwatuma.

Mhe. Mwenyekiti katika jambo ambalo silipendi ni kumtuma mfanyakazi halafu nikashindwa kupata maslahi yake. Kwa hivyo hili tumeliweka kwa nia njema kabisa hilo ndio la msingi kwa hivyo naomba aridhike na hilo.

Kuhusu suala la safari za nje Mhe. Mwenyekiti nimesema hapa kwamba tuna tatizo kidogo Zanzibar na suala la promotion na ukilinganisha na nchi jirani sisi tuko nyuma sana. Nitatoa mfano, promotion gharama za kuutangaza utalii kwa nchi jirani Kenya wanatumia dola ishirini na tatu milioni kwa mwaka, Mauritius wanatumia dola kumi na tano milioni kwa mwaka, Tanzania Bara wanatumia dola milioni kumi kwa mwaka. Seychelles wanatumia dola milioni saba kwa mwaka, Ruanda wanatumia dola milioni tano kwa mwaka.

Sisi tumepanga fedha hizi Mhe. Mwenyekiti kidogo sana kwa hivyo ninamuomba sana Mheshimiwa sahiba wangu bosi wangu Mhe. Jusa aone kwamba lengo letu ni kupanda juu kidogo kuona na sisi kwa kweli tungetamani na sisi tuwe na angalau one million dollar lakini 0.2 Mheshimiwa ni ndogo sana kwa kweli. Vijana wangu wanapata kazi sana na kwa kweli tunakosa masoko mengi ambayo yana *potential* ambayo wangeweza kuja watalii wenye tija.

Kwa hivyo naomba mimi badala kunambia ni nyingi aniombee nipate nyingi zaidi mwakani tuweze kuitangaza Zanzibar ulimwenguni.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti ingelikuwa fungu hili liko katika jumla ya maelezo ya promotion ningekubaliana nae kabisa Mhe. Waziri, mimi binafsi nimewahi

kuzifatilia hizo takwimu wakati fulani tulipokuwa Bungeni katika kulinganisha nchi mbali mbali na Tanzania. Lakini tatizo langu Mhe. Mwenyekiti ni kwamba tunaweka *emphasis* kubwa mno kwamba kutangaza ni safari.

Mhe. Mwenyekiti, ninafikiri Mhe. Waziri ni shahidi kwamba unapoangalia vyombo vya habari vya kimataifa kwa mfano *CNN, BBC* ni kawaida kuona nchi mbali mbali zina-sponser matangazo dakika moja tu na gharama yake si ndogo lakini *impact*, athari yake katika kutangaza duniani ni kubwa sana. Sasa Mhe. Mwenyekiti tatizo langu ni kwamba kwa kuweka empasis kutangaza utalii ni kuongeza safari za watendaji wa Kamisheni ya Utalii ndio penye tatizo napo. Na niliwahi kuchangia mwaka jana Mhe. Mwenyekiti nikasema viongozi wa Kamisheni ya Utalii wakati fulani kulikuwa kuna ugomvi kwa sababu ya kugombania safari, wale wakubwa wa Kamisheni, sasa imekuwa tija inayopatikana pale ni mtu kwenda kutafuta posho.

Sasa nataka niseme nataka nimkubalie tuendelee lakini nimuombe Mhe. Waziri katika utendaji kama alivyosema kuzidisha mafungu hapa na Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Fedha anafaham, haina maana kwamba zikatumeke hivi hivi, wana nafasi ya kwenda kuangalia mwisho tiba iliykuwa kubwa zaidi, hebu tukaangalie njia bora zaidi za ku-promote utalii wetu badala ya kila wakati watendaji wakuu wa Kamisheni ya Utalii kusafiri na kwenda kutafuta posho Mhe. Mwenyekiti. Ninashukuru sana lakini baadae nasema tuendelee naamini waziri wangu ninamuamini kwamba anaweza kuifanya kazi hii ya kufatilia njia bora zaidi za kuutangaza utalii wa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti ushauri wake ni mzuri na tutaufanyia kazi ninamuahidi.

Kifungu 0201	Utawala Unguja	1,105,108,000
Kifungu 0301	Afisi Kuu Pemba	212,892,000
Jumla ya Fungu		**1,318,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na
Kamati bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu nambari 42 Wizara ya Habari Utamaduni Utalii na Michezo, Makadirio ya Fedha yanayohitajika kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2012 kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo ni jumla ya shilingi 7,678,000 Wizara ya Habari Utalii Utamaduni na Michezo vifungu vya fungu hili vinavyooneshwa hapo chini matumizi yake yatasimamiwa na Katibu Mkuu Wizara ya Habari Utamaduni Utalii na Michezo.

Kifungu 0201

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana katika majibu yake Mheshimiwa wangu kuna suala amenisahau imenibidi mimi lazima nisimame, masuala mengi nimekubaliana naye lakini hili suala ambalo mwaka jana nilikuwa mkaidi sana katika Waziri aliyepita mpaka akachoka kunijibu. Suala la uchaguzi wa Chama cha Riadha. Mhe. Waziri bado hujanijibu na hili mimi sitokubaliana nalo kwa sababu Mhe. Waziri aliyepita aliniahidi na kwa bahati nzuri

mjumbe wake tulikuwa tunawasiliana kwa simu kwa kujiandaa kufanya uchaguzi na Katiba imeshaanza kurekebishwa lakini imefika katikati haijamalizwa. Je Mhe. Waziri hili utanambiaje?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti ni kweli Mheshimiwa sahibu yangu alizungumza suala hili na akanambia kwamba usipojibu vizuri hili mimi sikubali, sasa nilidhani kwamba nimemtosheleza. Ni kweli kwamba chama cha riadha ni miongoni mwa vyama kama vinne ambavyo miongoni mwa thalathini tulivyonavyo ambavyo havijafanya uchaguzi wake. Mrajis wa Michezo na Baraza la Michezo limewambia mara nyingi kwamba kuna umuhimu lakini wakasema hawana fedha. Baraza la Michezo likawasaidia kuwapa fedha kwa ajili ya kufanya mkutano mkuu wake. Kwa hivyo washarekebisha katiba yao sasa ni kweli, sasa iliyobakia ni wao wenyewe kujipanga.

Sisi kama wizara sasa kama Baraza la Michezo kwa mujibu wa sheria mpya tuliyoipitisha Barazani hatuna mamlaka ya kuingia ndani, kwa sababu kuna hofu kwamba tutaweka vibaraka wetu. Kwa hivyo ni juu yao kuhakikisha kwamba wanafanya uchaguzi. Sisi tunaendelea kuwahimiza na baya zaidi nimemwambia Mrajis awape ultimatum kama baada ya miezi mitatu basi tutafuta usajili. Sasa baada ya kuwapa hilo naona wameanza kuchangamka kidogo.

Kwa hivyo sisi tuko tayari kuwasaidia, lakini juu yao wenyewe kuhakikisha kuchangamka vyenginevyo tukisimamia sisi kwa mujibu wa sheria mpya ya Baraza la Michezo tuliyoipitisha itakuwa kwenda kinyume na sheria yenyewe. Wanatakiwa wenyewe vyama vijipange kama wanahitaji pesa ndogo ndogo kwa sababu bado ni vichanga vyama sisi tunavi-*support*. Kwa hivyo Mhe. Mshimba najua wewe ni mwanariadha mzuri ungependa sana chama hiki kiwe na uongozi. Naomba tushiriane mimi na wewe Mheshimiwa tuwahimize wafanye uchaguzi na niko tayari. Kwa hivyo wakati wowote Mhe. Hata Ramadhan hii kama yuko tayari kushirikiana nae katika kuwahimiza basi mimi niko tayari.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, mimi sahiba wangu nimekubaliana suala moja tu anambie tu ni lini? Hiyo tu basi kwa sababu kauli hiyo siku zote ninaipata. Mashirikiano niko tayari na kweli nitakukera sikuachi, pengine kama mimi nataka kugombea Mwenyekiti je, mfano tunachukulia. Lakini Mhe. Waziri naomba kauli yako ndogo tu unithibitishie, Mhe. Mshimba baada wiki moja au baada ya kumaliza bajeti yangu na tutakupitisha wala usiwe na wasiwasi. Mheshimiwa keshaanza hapa Mhe. Hamza kukurahisishia kazi na sisi tutakurahisishia kazi hebu nipe hiyo siku tu basi. Baada ya wiki moja, baada ya mwezi mmoja angalau na mimi niridhike Mheshimiwa, michezo tunaitupa. Juzi kaja mtoto hapa katuonesha jinsi gani tunashinda huko nje. Sasa Mheshimiwa kila siku mambo haya yatakuwa yanakwenda hivi na hivi nakuomba Mheshimiwa mtiifu kweli, hebu nipe angalau nikae mwezi, wiki utajua wewe.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti naogopa kutoa ahadi kwa sababu ingelikuwa ni suala la kusimamiwa moja kwa moja na watendaji wangu ningemwambia hata kesho. Lakini linahusu wao wenyewe, shughuli hizi sisi kama tuna-impose uongozi na ni kinyume na utaratibu wa chama chetu. Sasa mimi niko tayari hata kesho tunakaa nao mimi na wao tuwahimize, kesho jumamosi atanistahmilia tuna kikao serikalini. Lakini jumapili tukutane mimi na yeye na wao, tuwaambie tuwahimize lini wana shida gani, wamekwama wapi ili uchaguzi ufanyike sina tatizo na hilo lakini nataka kauli itoke kwao. Na

kama kuna matatizo madogo wamekwama basi Wizara itahakikisha kwamba inawasaidia uchaguzi wao unafanyika.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti ninashukuru sana tena sana ndio maana tukasema kwamba kuwa Waziri wetu huyu katika hesabu yetu ni mmoja ambaye anayekubali matakwa yetu yale tunayotaka kwa maslahi ya wananchi. Mheshimiwa mimi ninamuomba sana tuendelee lakini mimi nitakuwa chini ya ubavu na wewe.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia kwenye hoja hii niliwapongeza Wizara kwa kuandaa zabuni 12 na zabuni moja ikiwa ni ya mnara wa Chumbuni kuelekea Bungi. Nilitaka kujua kwa nini mnara haujamalizika na Mhe. Waziri amesema kwamba sababu ni ugomvi wa kampuni yenyewe. Sasa naomba kujua tu mkataba wetu unasemaje, mkataba ulizingatia huo ugomvi kwamba ukitokea ugomvi tuuachie au haukusema, kama haukusema Mhe. Waziri anisaidie hadi unatokea ugomvi kampuni ilikuwa imelipwa kiasi gani cha fedha na bado kiasi gani.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mhe. Hija alizungumza hilo na mimi nilijitahidi sana kulijibu, kwa taarifa nilizonazo na utafiti mdogo nilioufanya nimejitahidi sana kumjibu. Sasa kwa maelezo ya ziada ni kwamba, mkataba wa ujenzi ule wa mnara ulifungwa Septemba, 2011 na walitakiwa wawe washakamilisha baada ya miezi mitatu; Oktoba, Novemba na Disemba Januari wawe wamekabidhi. Mimi ilipofika Aprili haujamaliza na jambo moja ambalo Mheshimiwa mwenzangu alinikabidhi ni hili, kwa hivyo nikafanya ziara makusudi nikagundua kwamba mnara bado uko chini haujaanza kupanda. Aprili, Mei nikamwita mhusika nikamwambia mbona unafanya hivyo, ananambia aa, akanipa habari nyingi.

Lakini watendaji wenzake wa kampuni wakasema bwana sisi huyu tapeli na sisi hatukamilishi kwa sababu ameshatutapeli. Nikawaambia aa sikilizeni jamani, mimi habari hizo sijui, najua mkataba, lakini wakanambia kulikuwa na mvua na upepo maneno mengi tu, nikawaambia sasa nataka mnara umalize Mei. Ilipofika mwezi Juni sijawaona nikawachapa barua, barua nambari WHUMH1041Vol. 1192 ya tarehe 13 Juni, nikampelekea barua na nikauangalia mkataba, ili tumpeleke Mahkamani kwa mujibu wa mkataba lazima umpe *notice* ya siku saba.

Kwa hivyo, mimi nikaagiza kwamba apewe *notice* na akapewa, naomba nisome kibwagizo cha mwisho kwamba, kufuatia hali hiyo Wizara inakusudia kukupeleka Mahkamani kwa mujibu wa kifungu cha 7 cha mkataba huo. Kwa hivyo, wizara inakupa siku saba kuanzia tarehe ya barua hii utoe maelezo kwa nini umeshindwa kukamilisha kwa wakati, na kwamba kampuni yako itaweza kukamilisha kazi hiyo lini. Iwapo hutatoa maelezo ya kujitosheleza ndani ya siku hizo au kama wizara itaona maelezo yako sio ya msingi itachukua hatua za kisheria dhidi yako. Alipoipata barua hiyo akakurupuka ghafla akaja ofisini na maneno mengi lakini baadae akajibu barua ndefu na *paragraph* ya mwisho akasema nanukuu kwamba;

“Kwa mantiki hii naomba kutoa ahadi kuwa kampuni yangu bila ya kuchelewa itaweza kufikia hatua ya mwisho ya kumaliza ifikapo tarehe 30 Julai, 2012 kwamba naamini ikifika tarehe hiyo kazi nitaikabidhi. Kwa maana hiyo iwapo tarehe hiyo itafika na kwamba hakuna kazi ya hatua ya mwisho kufikiwa au kukamilika mnara huo basi niko tayari wizara yako kuipeleka Mahkamani

kama ulivyosema katika barua yao. Naomba kuahidi kwa udhati kabisa kuwa Kampuni yangu ina nia ya kukamilisha kazi hiyo pamoja na yote. Nitashukuru sana kama ofisi yako itanikubalia ombi langu natanguliza shukurani za dhati kwa mashirikiano hayo".

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa barua yangu hii na kwa jibu lake hili nikamuona ameanza kuja na watu wake wameanza nikawauliza vipi wakasema tunakuja. Na kwa kweli nashukuru kuanzia wakati huo juzi saa 12 jioni mimi nilikuwa Bungi nikaona kwamba vimepandishwa vipande 17, jana wamepandisha kipande kimoja ile kazi ni ngumu sana Mhe. Mwenyekiti, ni ngumu na siku hizi kuna upepo ni mtihani kidogo lazima tuangalie ubinadamu na mambo mengine. Lakini wanafanya kazi nzuri na tarehe 30 Julai naamini kwamba ahadi yake ataikamilisha.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri kwamba kuna barua ndefu ambayo kampuni ilipeleka na kule mwisho alitusomea kwamba yuko tayari kumaliza mwezi huu wa saba. Lakini kama Waziri hebu atwambie huo ugomvi mpaka ukafikia ugomvi, mpaka akaitwa tapeli kwa wafanyakazi wake imetokana na nini. Kwa sababu taarifa ambazo zipo ni kuwa hakulipwa fedha zake, sasa ikiwa mkandarasi hata wafanyakazi hawatoweza kufanya kazi. Sasa hilo Waziri anasemaje je, pesa walilipwa kwa wakati? Kwa sababu asiitwe tapeli kumbe hakulipwa. Kwa hivyo atwambie je, kalipwa na kwa wakati gani, kama kalipwa si huyu tayari mkataba atakuwa ameuvunja, kama mkataba ameuvunja si kuna adhabu za mkataba.

Kwa sababu kama serikali ndio iliyofanya kosa kampuni wangetupiga *penalt* pengine kama yeye. Kwa mfano kalipwa hebu atwambie kalipwa kwa wakati, na kwa nini serikali ikakubali baada ya miezi mitatu sasa ni mwaka maana yake Septemba mpaka Julai ni karibu mwaka, kama kosa lingefanywa na serikali si kungekuwa kuna hasara, Hebu Mhe Waziri tuambie mmemlipa kwa wakati au waligombana bila ya sababu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, mimi sikuwepo wizarani, lakini nilipokuja nilijaribu kufanya utafiti, utafiti niliougundua ni kwamba kwa mujibu wa mkataba niliouona ninao ni kwamba, alitakiwa kulipa asilimia 50 baada ya kusaini *contract.* Humu imo risiti 0378 *from New Technical Construction* ya Dar es Salaam, *received from* Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo hiyo tarehe 19 Septemba P.O. Box 117 *Zanzibar Broadcasting Corporation 199 millions only, Central payment deposit account Num. 982015 demolish and eraction of must 120 meter Y.* Kwa hivyo, hapa walilipwa.

Halafu mkataba unasema kwamba, *25 percent of the contract once after the completion of 50 percent of the work.* Nafikiri *50 percent the work* walikubaliana akishaushusha. Kwa hivyo, humu imo risiti nambari 0379 *from New Technical Construction Company Ltd* kwamba *received from* Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ya tarehe 3 Novemba *Broadcasting Corporation* kwamba amelipwa shilingi 199 milioni kama ni asilimia 25.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi nimejiridhisha kwamba *instalment* mbili za mwanzo keshalipwa, *instalment* ya tatu siwezi kumlipa mpaka niuone mnara uko juu na ndio mkataba unavyozungumza.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwamba serikali imetimiza wajibu wake, lakini inaonekana serikali hiyo hiyo ilichagua kampuni zisizo na uwezo. Sasa Mhe. Waziri

aniridhishe hili anasemaje. Hii kampuni inaonekana si kampuni ambayo ina sifa, ni kampuni ambayo ilikusudia kutubabaisha, haiwezekani mamilioni ya fedha yalipwe kampuni ipewe miezi mitati sasa hivi ikaribie mwaka. Mhe. Waziri twambie kwenye mambo haya ya kampuni ya kazi hii waliomba watu wangapi na kwa nini mkampa huyu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilihoji suala kama hilo, kwa sababu mimi na Mhe. Hija tuna uzoefu mmoja katika masuala ya *PAC* kama alivyozungumza. Kwa hiyo tunajua namna ya kufuatilia mambo, alikuwa mwenzangu sana na mpaka leo ni mwenzangu sana. Kwa hivyo, nilihoji na nikagundua kwamba kuna kampuni tatu ziliomba, atanisamehe kwamba hilo faili zima sikulichukua, sasa nikauliza kwa nini kapewa huyu?

Jibu, kwa sababu ule mnara uliokuwepo Chumbuni kila mara ulikuwa unafanyiwa *painting* muda baada ya muda, sasa huyu mara zote kampuni yake ndiyo iliyokuwa ikileta watu kufanya ile *painting.* Kwa hivyo, ana uzoefu katika suala hili na kwenye mnara ule. Sasa hata katika barua hii niliyoisoma kuna ushauri wa mafundi wa *ZBC Radio* kwa sababu na wao walitakiwa ushauri tufanyeje, wao wakasema hivi, Katibu Mkuu wa Wizara. Kabla hajapewa ushauri kuhusu mnara wa Chumbuni, kwa heshima naomba uhusike na mada iliyopo juu, kwa ushirikiano wa pamoja baina ya Fundi Mkuu wa STZ wakati huo, Ndugu Ali Abuu Talib na Fundi Mkuu wa Kituo cha MW Ndugu Hamada Issa; tumefikia muafaka kwamba Kampuni ya *New Construction Ltd* ni kampuni sahihi ya kufanya kazi iliyoainishwa hapo juu.

Tumeutoa ushauri huu kwa kuwa *engineer* aliyekuja kuwakilisha kampuni hiyo ni *engineer* aliyefanya kazi ya kuusimamisha mnara huo hapo awali. Kwa vile kwa mara ya kwanza alifanya kazi hiyo kwa ufanisi mkubwa, imani yetu kuwa ana uwezo mkubwa wa kuifanya kazi hiyo kwa mara ya pili, tunategemea ushauri wetu huu utazingatiwa, tunategemea mashirikiano mazuri. Haya maneno ya mafundi, na hii kazi ya kiufundi Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, ilikuwa ni busara sana kuzingatia ushauri wa kiufundi katika kuipa nafasi kazi hii ifanywe.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri amesema kwamba tuna uzoefu mimi na yeye na mimi namuamini na nazidi kumwambia kwamba awe makini, lakini inaonekana kuna tatizo, sasa kwa sababu nyuma yangu kuna *PAC,* na *PAC* ndio inayoshughulikia suala zima la manunuzi na matumizi nadhani mwezi wa tisa wataliangalia hilo suala; hivyo tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia ukurasa wa 57 nikazungumzia kuhusu Hoteli ya Bwawani na nikasema ni *asset* kubwa kwa serikali, na hoteli hii imebeba historia kubwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Nilitaka kujua kutoka kwa Mhe. Waziri niliuliza kuna ofisi ngapi zimepangishwa kule chini, na kwa gharama gani, na kwa mkataba wa muda gani.

Vile vile kuna wafanyakazi wameajiriwa kwa muda mrefu haipungui miaka 14 mpaka 20, kwa masikitiko makubwa sana na kwa unyonge wa hali ya juu hivi sasa wale watu wanapewa mkataba wa miezi sita. Nini hatma yao Mhe. Waziri na haki zao zitakuwaje ukizingatia ni watu masikini sana Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, sikumsikia vizuri Mhe. Jaku anazungumzia suala la Bwawani au.

Mhe. Mwenyekiti: Anazungumzia Hoteli ya Bwawani ndio.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Hoteli ya Bwawani Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli nimesema labda alikuwa na udhuru unajua mtu mzima huyo mara hutoka nje. Lakini hakuna mfanyakazi ambaye ana mkataba wa muda, nimesema hapa kwamba wafanyakazi 125 wote kabla Mhe. Abdillah Jihadi hajaondoka, alihakikisha kwamba wameajiriwa na mimi nimefuatilia wameajiriwa, kwa hivyo sasa hivi wako katika *probation* wanamaliza miaka yao kwa mujibu wa sheria ya utumishi tayari wanaendelea na kazi. Kwa hivyo, hakuna ambaye amesema hapa, lakini labda alikuwa amedharurika kidogo unajua mawazo ya mtu mzima.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hatuna tatizo na Mhe. Waziri, kama alivyozungumza ni sawa mimi niko tayari kumletea wafanyakazi tuje tukae pamoja ili tupitishe. Mimi sina tatizo huu ni mwezi wa Ramadhani siwezi kuja kusema kitu nisichokuwa na uhakika nacho Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Tunashukuru tunaendelea lakini tuzingatie sana muda, kwa sababu kuna muda wa saa moja na dakika kama tano tu kumaliza.

Kifungu 0201 – Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	115,000,000
Kifungu 0301 – Afisi Kuu Pemba	590,506,000
Kifungu 0401	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, niliibua masuala mengi katika idara hii kuhusu matumizi mbali mbali, lakini kwa sababu ya umuhimu wa suala hili naomba hayo niyaache tutawasiliana na Mhe. Waziri baadae. Lakini kuna suala moja nililizungumza hapa ambalo nilitaka anipe maelezo lakini sikulisikia, suala la udhalilishaji wa wafanyakazi katika mahoteli ya kitalii na nikataja kesi maalum ya kadhia iliyomkuta kijana Suleiman Makame tarehe 11/07/2012 ambapo raia wa Mauritius anaitwa Vadvela Namswami akiwa ndio bosi wa sehemu ya ***pastries*** alimpiga mfanyakazi huyu na kwamba mfanyakazi huyu alikwenda polisi akachukua *PF3*, lakini tangu ameripoti suala hili kumekwenda kuhojiwa wafanyakazi lakini hakuna hatua iliyochukuliwa.

Kwa hivyo, kumekuwa na kesi nyingi tunazoripoti hapa kama anakumbuka Mhe. Waziri niliwahi kumwambia katika mchango wangu katika hoteli hii hii msichana mmoja aliwahi kudhalilishwa mpaka kuvuliwa nguo.

Tulilizungumza katika Baraza hili katika vikao vilivyopita sasa hii hoteli inaonekana ni *notorious*, inaendeleza vitendo hivi vya udhalilishwaji wa Wazanzibari ambapo sisi kama wawakilishi wao Mheshimiwa hatuwezi tukavikubali. Kwa hivyo, nilikuwa naomba hili anipe kauli yake Mhe. Waziri anachukua hatua gani kuwasiliana na uongozi wa hoteli hii na nyengine ili kukomesha vitendo kama hivi vya udhalilishaji kwa vijana wa Kizanzibari ambao wanafanya kazi katika sekta ya utalii. Tunaipenda sekta ya utalii, tunataka tuongeze mapato lakini sio kwa gharama ya kuwadhalilisha Wazanzibari katika nchi yao.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na naelewa *concern* ya Mhe. Jussa katika suala hili, na nilipokuwa nazungumza pale nilisema kwamba hata mimi suala hili linaniudhi na nilisema kwamba Zanzibar ni nchi na ina wenyewe na wenyewe ndio sisi, hatuwezi kuacha mambo haya yakaendelea. Nilichokuwa naomba na bado namuomba Mhe. Mwakilishi wa Mjimkongwe na Wawakilishi wengine kwamba masuala hayo yakitokea tuarifiane ili tuchukue hatua mapema tusikae sana.

Ningelitoa mfano kuwa, nilisikitika jana kusikia swahibu wangu Mhe. Mwenyekiti wa *PAC* wametomeshwa mbwa hotelini, hilo si jambo zuri na kwa kweli kama angenambia mimi siku hiyo hiyo, labda iwe sijafika lakini kama nimefika ningekwenda kwa Mhwa. Waziri wa Kazi, Maalim Haroun tukamshughulikia hapo hapo. Lakini sasa ni vizuri tuambiwe wakati shughuli hizi zikifika ili sisi Kamisheni ya Utalii na Idara ya Kazi tuweze kufanya ya kuwaadabisha wale ambao wanafanya hivyo. Kwa hivyo, sisi katika serikali Mhe. Mwenyekiti, hasa katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo mambo haya tunayalani na tunaahidi kwamba tukipewa wakati muwafaka basi hakikisha kwamba Wazanzibari wana mtetezi madhubuti. Naomba hilo Mhe. Mwenyekiti, tushirikiane tupewe taarifa.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, ni majibu mazuri sana Mhe. Waziri ameyatoa lakini naomba niongezee kidogo tu. Kwanza hapa pana ahadi ya yule Meneja wa hoteli ile au mdhamini kwamba kosa kama lile halitatokea tena. Sasa hapa limetokea, kazi yetu sisi kama Wizara ya Kazi tulifuatilia kwa makini kabisa tutamshauri huyo mhusika aje ili tumpeleke kwenye Kitengo cha *DHU*, *Dispute Handling Unit* ili hatua za kisheria zichukuliwe. Kwa sababu kwanza keshahalifu ahadi yake ambayo alinipa mimi mwenyewe kwamba hili halitatokea tena na madhali limetokea tena mimi nitalisimamia kwa nguvu zangu zote kwa kushirikiana na Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo suala hili.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti nashukuru, kwanza nataka nimhakikishie Mhe. Waziri kwamba hata hii tarehe niliyompa ni tarehe ya karibuni sana, kwa hivyo na mimi nimelipata katika mazingira wakati tuko kwenye kikao hiki ndio maana nimelileta hapa, lakini kama si hivyo ningewasiliana nae. Anajua mara nyingi yanapotokea baadhi ya mambo huwa tunawasiliana kwa sababu hatupendi kuwa kila jambo lije hapa. Kwa hivyo, nashukuru. Pia nashukuru ahadi ya Mhe. Waziri wa Kazi ambaye pia nampongeza ni mmoja katika wafuatiliaji wazuri tunapompa masuala yetu, bahati nzuri ninayo hata nambari ya simu ya huyo kijana kwa sababu kanambia yuko tayari kuhojiwa na kutoa maelezo popote tutakapomkuta. Kwa hivyo, nitayafikisha kwao ili wahusika wawasiliane nae na suala hili lichukuliwe hatua kama alivyosema ili kusiendelee na unyanyasaji kama huo. Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa upande wangu nasema tuendelee.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nilihoji katika kifungu hiki maslahi ya wafanyakazi wetu waliokwenda nchini Uholanzi kwa ziara za kikazi na mafunzo. Mhe. Waziri hoja yake kubwa ni kwamba amenukuu kanuni ya fedha kwamba kifungu cha 93 hakiruhusu mtu kulipwa bila ya *supporting document* na mimi nakubali, kwamba huwezi kulipa fedha bila ya vielelezo. Lakini taarifa ambazo ninazo wafanyakazi hawa hawakutoka tu kinyemela walikwenda kwa

idhini ya wizara na kwa hivyo tiketi na maandalizi yote ya wizara yalikuwa yanajulikana na yapo.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana Mhe. Waziri aliyepita hakuwa na hoja hii yeye alisema kwamba tatizo kubwa ni fedha kwa hivyo aachiwe bajeti ijayo na fedha itapatikana. Kwa hivyo kama ni tatizo la *document* zimepotea basi kanuni hii kifungu cha 65 kinatoa adhabu kwa yule afisa ambaye amepoteza *document* za ofisi, kwa nini asimuadhibu ofisa wake aliyepoteza *document* za ofisi na awaadhibu wafanyakazi ambao wametumwa. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema kwamba ikiwa hoja ni fedha tupunguze kasma ya 220301, 220302, 220305 Safari za Nje shilingi milioni mia moja tuwape fedha zao shilingi milioni ishirini kwa sababu watu wengine wamekufa. Zipunguzwe shilingi milioni ishirini kwenye mia ili wasende nje kwanza tuwalipe wale marehemu wengine wana warithi wao ili hii haki itendeke, hatuwezi kwenda katika kuwaonea wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu tupunguze shilingi 20 milioni kwenye mia ili wale wanaokwenda nje wasiende kwanza tuwalipe hawa marehemu ili haki ya watoto wao ipatikane. Mhe. Mwenyekiti nashukuru.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli nimemsikia sana Mhe. Hija, tatizo si pesa, mimi ningelikuwa tutapata *supporting document* hata leo najua sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais angenikopesha ili kuondoa hili tatizo, lakini tatizo ni *supporting document.* Sasa mimi ninachomuomba mimi nimekuja wizarani juzi tu anipe nafasi kidogo tupitishe bajeti, wenyewe niliwaahidi hivyo wanipe nafasi tupitishiwe bajeti fedha tunayo, niandae utaratibu ikiwezekana hata kumuona Waziri wa Fedha lakini tupate ruhusa.

Kwa sababu Mhe. Hija sheria tukishaitunga lazima tuiheshimu, sasa naogopa kwamba mimi ni waziri ambae sheria hii nilikuwepo katika kuitunga lakini leo nakwenda nayo vibaya. Kwa hivyo, ama nizitafute *supporting document* au nitafute taratibu nyengine kwa kuhalalisha malipo. Naomba waniamini kama ambavyo wameniamini kwa mambo mengine nitahakikisha tukijaaliwa utaratibu unafanywa pesa zao zinapatikana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, hili nadhani si la Wizara ya Fedha, *supporting document* ya kwanza ni *ticket, passport, visa* zote hizo zipo na wanazo; hata hao ambao walifariki itakuwa *passport* zao huko kopi ziko. Sasa si tatizo la *supporting document* ninachosema kwamba hili suala si la Wizara ya Fedha hizi shilingi 100 milioni waziri akubali tukate shilingi 20 milioni wapewe haki yao, leo wafanyakazi wetu wanadhalilika.

Mhe. Mwenyekiti, si wafanyakazi wa wizara yake tu, alichukua mpaka Baraza la WAwakilishi wengine humu kwa sababu wandishi wa habari, mpaka mfanyakazi mwandishi wa Makamu wa Pili wa Rais ofisi yake. Sasa si tatizo la *document* kwamba kuna utashi hawataki kulipa hivyo tuwazuwie hawa maafisa wasiondoke, kwanza tuwalipe hawa wafanyakazi wetu na kuna mwandishi mmoja wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kuna mwandishi mmoja Baraza la Wawakilishi na waandishi wengine katika ofisi yake. Hatuwezi kufanikiwa kwa mwaka mzima, waziri aliyepita alitwambia fedha hakuna, leo anatwambia *supporting document*, kesho

atatwambia *printer* imekufa. Kwa hiyo pesa zikatwe tuwalipe wafanyakazi na wao wakose kwenda nje.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, hata ukizikata labda uzirudishe Wizara ya Fedha, lakini kama utarudisha ofisini kwangu bila ya *supporting document* sitaki kutafuna maneno hilo haiwezekani, lazima tufuate utaratibu wa sheria iliyopishwa hapa. Sasa kama wanazo niletee nitalipa kama ambavyo nimelipa nyengine, lakini kwenda kinyume na sheria hii Mhe. Mwenyekiti, haiwezekani na yeye mwenyewe anajua tulikuwa tunaisimamia kwa wenzetu leo siwezi kwenda kinyume na hayo. Kwa hivyo, kama vijana, kama wafanyakazi wana supporting document niko tayair kulipa tukijaaliwa mara Waziri wa Fedha atanipitishia, lakini vyenginevyo Mhe. Mwenyekiti, kwenda kinyume na sheria hii kama wenzangu walipewa basi mimi nipewe ili nilipe.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema kwamba asiwaadhibu wafanyakazi wa kawaida, kama *document* zimempotea ofisa wake ndiye aliyepoteza na kama anafuata sheria hii basin na afuate kanuni ya 65 amuadhibu ofisa wake waliyempa dhamana akashindwa kusimamia ndivyo inavyosema kanuni hii, asiangalie kulipa tu aangalie na uwajibikaji. *proparly code* kwa nini akashindwa kuweka kumbukumbu ofisa wake neo lenye shilingi milioni mia moja na mara hii akose pia kumbukmbu. Kwa hivyo labda Mhe. Waziri anambie mimi mwenyewe nikampe kumbukumbu na tuwaite tuwalipe wafanyakazi haka sana iwezekanavyo.

Kwa sababu tukiwaacha hapa Mhe. Mwenyekiti hawalipi na hawalipi si kwa sababu hawataki kama waziri, kuna watu wanaona kam aile kazi imwisha, watu wamekopa shilingi mbilioni tano, wengine sita kwa hivyo tufanyeje Nge. Mwenyektikwa hivyo, Mhe. Waziri labda atwambie kwamba mimi nitoe kumbukumbu fedha hii akubali kmwaba tuikate baada ya kupelekewa kumbukumbu atizame siku ya Jumatatu na mimi nitamletea kumbukumbu, lakini kama umeshindwa kuripoti kumbukumbu maafisa wake kwa nini tuombe shilingi miliongi mia moja nyengine.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimuombe sana ndugu yangu, mdogo wangu Mhe. Hija atuachie hili suala tulitizame kwa pamoja, ofisi yangu, Ofisi ya Utumishi wa Umma na Wizara ya Sekta. Kwa sababu kuna taratibu za mtumishi anapokwenda mafunzoni mpaka aweze kulipwa na serikali, tutizame vile vielelezo vyote kama vipo na ni sahihi na mtumishi huyu amekwenda kwa ruhusa ya selikali na vielelezo vyake vyote vipo basi nadhani aturuhusu sisi tutafanya hizo taratibu nyengine zilizosalia. Aruhusu hiki kifungu kipite ili sisi wizara tatu tuja tukae na tulichunguze kwa undani kabisa, hapa nadhani watakuwa wanavutana na Mhe. Waziri kwa sababu kwanza lazima tukubali Mhe. Waziri ni mpa na hilo sala limetokea muda mrefu lakini vile vile kuna taratibu za kiserikali lazima Mhe. WAziri azisimamie.

Lakini vile vile nakubali kwamba Mhe. Hija naye anawasimamia wananchi kwa hivyo mimi nakuomba sana, turuhusu hili fungu lipite na tutalifanyia kazi na katika kipindi kifupi tutakupa majibu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi namuamini sana Mhe. Waziri wa Fedha, lakini naomba kitu kimotu, akubali kwamba wakati Kamati yake ya Mifugo inapokwenda

kwenye *site* muda huo iwe tayari watu hao wamelipwa. Sijui nimefahamike, naomba Kamati yake ya Mifugo itapokwenda kwenye wizara mwezi wa tisa iwe tayari hili suala wamelimaliza, akikubali hilo tukijaaliwa tuendelee.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimhakikishie tu Mhe. Hija *once* taratibu zikishakukamilika basi hilo tutalizingatia kwa ukamilifu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine tena naendelea kumshukuru au kumpongeza Mhe. Waziri kwa jinsi anavyojitahidi. Katika nilipokuwa nikichangia nilielezea suala la wale wafanyakazi wa redio ambao wengine wapo muda mrefu wanafanya kazi wameshaandika taarifa nyingi na taarifa zao zilikuwa tayari zinakubaliwa na wizara na zikawa zinatumika katika shughuli mbali mbali. Lakini ulipofika wakati wa uajiri wametafutwa watu ambao hawana hata uzoefu wa kazi wale wengine wamekwenda kufanyishwa *interview*.

Mhe. Waziri nimefuatilia alipokuwa akinijibu alinielezea kwamba tumepitisha Sheria ya Utumishi wa Umma ni kweli tunakubali, lakini kwa kuwa tumepitisha sheria ya utumishi wa umma lakini vile vile sheria na huruma. Sheria na huruma yenyewe inavyokuja kwamba tayari kuna mtu keshakufanyia kazi miaka sita hujamtoa kasoro katika taarifa zake unakwenda kumchukua mtu nyumbani anakuja kufanya *interview* yule ambaye yuko pale unamuacha na hii *interview* imeshafanyika.

Sasa nilikuwa namuomba Mhe. Waziri kama tunavyomsifu kwamba ni mfuatiliaji tunaomba kwanza hili zoezi alisimamishe la kutoa matokeo awaite wale wahusika waangalie viel vigezo walivyochukua, kwa nini hawa wengine wakawaacha wasiwafanyishe hata *interview* ambapo wameshasota zaidi ya miaka mitano au sita. Baada ya majibu yake nafikiri nitakiruhusu kifungu kiendelee kama atanitosheleza. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti, Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura alizungumza hilo na *concern* yake naifahamu. Kwa hivyo, nakubali kwamba ushauri wake kuzuia hili suala la matokeo, lakini pia namuahidi kwamba nitashauriana na Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuangalia namna gani ya kuwasaidia hao.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naendelea tu kumpongeza Mhe. Waziri, lakini yule mtu wa kufanya hizi saini tunamuomba aendelee isiwe kwamba baada ya wizara yake tena ikawa basi, yule pale mdogo anaefanya saini. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri nadhani hili kweli mtusaidie kwa sababu nakumbuka ipo hoja ikaambiwa tena tulipewa sisi kwamba Baraza hebu tutafutieni wale watu wanaofanya saini, sasa leo amemuona pale. Nadhani tukubali kwamba tushirikiane na uongozi wa hapa ili hilo jambo tuliweke.

Kifungu 0401 – Utumishi na Uendeshaji	1,275,920,000
Kifungu 0402 - Chuo cha Habari	305,000,000
Kifungu 0403	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nazingatia sana muda naomba maelezo mafupi tu ili turuhusu tuendelee. Katika mchango wangu Mhe. Waziri atakumbuka kwamba nilisema kuwa bajeti ya ruzuku kwa ajili ya Shirika la Magazeti ya Serikali ukiangalia miaka miwili iliyopita limeongezeka sana kutoka miaka hiyo, na nikasema sasa tatizo kwa sababu ubora wa gazeti tunaliona mabadiliko yake. Lakini nilitaka anipe maelezo kwamba, kwa sababu katika hotuba yake amesema wameongeza sana vituo vya uuzaji na usambazaji wa gazeti hili, nilikuwa naamini kwamba hiyo pia itakuwa bila shaka imeongeza mapato kwa shirika hili kwa sababu hasa hata Wazanzibari bila ya kujali itikadi zao wanalisoma kwa wingi Zanzibar Leo pengine kuliko gazeti jengine lolote. Kwa hivyo, nilikuwa nataka anisaidie kwamba je, haya mapato yameongezeka kiasi gani na kwa nini tuendelee kuidhinisha fedha hizi nyingi za ruzuku ikiwa shirika nalo linaongeza mapato yake. Hebu aniweke sawa katika hilo ili tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mhe. Jussa alizungumza hilo na sikumpa maelezo na ninamuomba radhi kwa hilo.

La msingi ni kwamba Shirika ni kweli kwamba linaonekana ruzuku yake inakua lakini naomba anifahamu kuwa katika kitabu changu bado pia nimesema kwamba shirika lina mpango wa kuongeza kwanza ukubwa wa gazeti, lakini pia kuongeza gazeti jengine la michezo.

Kwa hivyo naomba akubali kwamba bado Shirika halijapata ufanisi mkubwa. Tuna mambo mengi bado yanaendelea kupata ruzuku, kama nilivyozungumza hapa hatujakuwa na jengo letu. Kwa hivyo Mhe. Mwakilishi naomba akubali kwamba bado serikali iendelee kulilea shirika mpaka hapo litakapojiweza ndipo hapo nitakapoweza kulipunguzia ruzuku zake. Lakini kwa wakati huu kwa kweli kile ambacho kinakusanywa pamoja na shughuli nyingi sikuweza, naomba radhi sikuweza kuki-*comply* chote lakini bado hakitoshi kwamba shirika liweze kukatiwa ruzuku yake.

Tuna mambo mengi kama nilivyozungumza lazima ni wakati sasa wa gazeti hili kuwa na gazeti zaidi ya moja, kwa sababu kuwa na gazeti moja ni mtihani. Kwa hivyo haya ndio sababu tunaendelea kupata ruzuku kubwa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ninapokea maelezo yake niombe tu Kamati inayoongozwa na *iron lady* Mhe. Asha Bakari Makame, kamati inayosimamia wizara hii wafuatilia kwa makini kuona kwamba kuna mapato yanatoka basi yanasaidia kuliboresha shirika zaidi.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mwenyekiti mwenye chuma cha pua (*Kicheko*).

Kifungu 0403 Mchango wa Gazeti la Zanzibar Leo
shs.856, 000,000/=
Kifungu 0404

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, asione taabu Mhe. Waziri kila nikisimama mimi huwa ninamfanyia CV zake ziwe nzuri.

Nilisema hapa kwenye Chuo cha Utalii kuwa kipewe hadhi yake na kisaidiwe lakini nimeshtuka kuona hili fungu mwaka jana milioni mia mbili, leo ninaona milioni thamanini nne. Sasa nimeshtuka na ile hoja yangu kuwa kithaminiwe, kiendelezwe, halafu leo ninaona yanazidi kuwa nyuma. Kidogo naomba Mhe. Waziri anisaidie ilikuwaje mwaka jana milioni mia mbili leo thamanini na nne. Naomba kidogo tu aje anisaidie.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Mshimba alisome fungu lote. Fungu la mwaka jana lilikuwa ni milioni mia nne na mwaka huu ni milioni mia nne na ishirini.

Kwa hivyo zimeongezeka hazikupungua. Kwa hivyo naomba aliangalie hivyo lakini pia Chuo hiki kina mradi mwengine wa maendeleo wa milioni mia nne tutauona mbele huko. Kwa hivyo tunakisaidia na juzi Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ninamshukuru alikwenda pale kuzindua jengo zuri ambalo limesaidiwa na serikali na lengo letu ni kuona kwamba Chuo kile baada ya muda mfupi kimefika kutoa digrii angalau ya kwanza na ya pili kwa ajili ya shughuli za utalii hapa Zanzibar.

Kwa hivyo tupo karibu nacho sana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nilichokusudia mimi kunako hii ruzuku kwenye uendeshaji. Lakini kajibu uzuri Mhe. Waziri ninakuachia tuendelee.

Kifungu 0404 Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar	shs.420, 000,000/=
Kifungu 0701 Idara ya Habari Maelezo	shs.268, 630,000/=
Kifungu 0702 Tume ya Utangazaji	shs.168, 000,000/=
Kifungu 0703 Idara ya Habari Maelezo Pemba	shs.25, 000,000/=
Kifungu 0704	

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nilivyokuwa ninachangia nilizungumzia suala zima kuhusu ile kampuni iliyokuwa imeunga umeme kule Masingini. Mhe. Waziri amejaribu kulijibu hili suala lakini kidogo limekuwa lina utata.

Maana tulipozungumza tuliwaita sisi wale watendaji wa shirika hili na wao walitueleza ndio kwanza wameiona hiyo habari pale, hawana taarifa yoyote. Kwa hivyo tuliwataka watupatie taarifa, baadae wakatujibu kwamba wanalifuatilia.

Tukawafuatilia tena wakatwambia kwamba yule mtu kaunga tu kinyemela pasi na kufuata na utaratibu wowote ule. Lakini Mhe. Waziri alipokuwa anajibu hapa anasema kwamba kulikuwa kuna mkataba kabisa baina ya yule muungaji pale na shirika hili.

Sasa mimi nilikuwa mkataba ule ulifungwa lini, na nilikuwa ninataka niuone kama mkataba huo upo kweli na umefungwa lini na kwa makubaliano gani. Maana anachosema yeye kutoa umeme kwa kupewa *internet*. Lakini ule umeme uliungwa baada ya yeye kukatiwa. Sasa tulipokwenda

pale Mhe. Waziri kweli yeye alitoa agizo pale kwamba ule umeme uondoshwe ulichomolewa kwenye ile *switch*. Sisi tulipokwenda tukaukunja na waya wake kabisa tukaondoka nao.

Sasa nilikuwa ninataka maelezo ya ziada. Maana yake sijafahamu ule mkataba wa kutoa *internet* kwa muda gani na ule mkataba kama upo pia nilikuwa naomba kuuona Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, labda Mhe. Mtando hakunifahamu vizuri.

Nilichosema ni kwamba maelezo niliyopewa ni kwamba Zanlink ipo pale siku nyingi mnara wao pale. Sasa walikuwa na makubaliano na sio mkataba. Nikauliza hata na mimi muna mkataba wa maandishi kabla sijatoa kwa sababu nisingeweza kutoa amri kwamba ukateni, kama pangekuwa na mkataba *of course* ingekuwa na hiyo.

Sasa nilipouliza nikaambiwa pana makubaliano ya mdomo, nikasema ya mdomo ukateni sasa hivi. Kwa hivyo mimi nilipoambiwa pana makubaliano ya nipe nikupe ya mdomo, nikasema hatuwezi kuendesha nchi katika masuala ya *internet* kwa mdomo. Kwa hivyo sijasema mkataba nilichokusudia kwamba ni makubaliano ya mdomo kwamba wao watatoa umeme, wao watawapa vipindi kupitia Zanlink kwa ajili ya *network*, hayo makubaliano ya nyuma.

Lakini mimi nilitoa amri kwamba kateni na ulikatwa na mpaka leo haujaungwa tena. Kwa hivyo hayo ndio maelezo ninayoweza kuzungumza.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya Mhe. Waziri yamekuwa yamebadiliko kidogo kuliko yale ya awali. Maana nilivyofahamu mimi aliposema makubaliano, ninachofahamu mimi maana yake ni mkataba kwa sababu hii ni taasisi ya serikali na hii ni ya mtu binafsi.

Sasa kama kuna makubaliano ya mdomo, sisi tutayaelewa vipi na kile kinachotumika pale ni fedha za wananchi kwa sababu ule umeme unaotoka pale unalipiwa kutokana na kodi za wananchi.

Sasa kama kuna makubaliano ya mdomo kwa kweli kama huo ndio utaratibu wa kiserikali sielewi labda Mhe. Waziri anisaidie hapo kidogo ndio utaratibu wa kiserikali huo kwamba mnafanya makubaliano ya mdomo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, sio utaratibu na ndio maana nikatoa amri ukatwe kwa sababu sio utaratibu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa sio utaratibu nilikuwa naomba hatua ambazo amechukua kwa wale maofisa walioshughulikia suala hilo, kwa sababu wamekiuka utaratibu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, sikuona umuhimu wa kuchukua hatua kwa sababu suala hili ni la siku nyingi ambapo watendaji wale wa sekta binafsi na iliyokuwa Televisheni Zanzibar walikubaliana kwa mdomo

kubadilishana *service*, yule kutoa *service* ya umeme aliyonayo pale karibu, kwa hivyo sikuweza tena kusema kama kuna hatua yoyote ni nani *of course* hata yule aliyekuwepo siye, kwa hivyo ingekuwa ni wakati mkubwa labda wa miaka mitatu minne mitano nyuma pengine kumi. Kwa hivyo sikuona umuhimu nilichoona umuhimu ni kuhakikisha kwamba utaratibu huu wa sheria unasitishwa na ninafurahi kwamba ulisitishwa.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi ninashangaa kidogo Mhe. Waziri anaponiambia kwamba hakuna umuhimu wa kuchukua hatua wakati ameona kuna kosa. Sasa kama kuna kosa halafu hatua hukuchukua Mhe. Mwenyekiti, mimi ninapata tabu kidogo hapa.

Kwa sababu fedha zinazotumika katika kuchukua ule umeme ni fedha za serikali na za wananchi zile. Sasa kama kuna mtu kasababisha uzembe ule ukawa unatumika umeme ule wa ovyo, kwa hivyo hii anasema anatupa *internet* hatuna uhakika ni kitu cha uongo mimi ninaweza kusema kwa sababu hakina ushahidi wowote kwamba anatupa *internet*, hatuwezi kupewa *internet* huku ukitazama hata kaika hesabu zao kwenye mafungu haya, kuna fungu tunaidhinisha kwa ajili ya mtandao.

Sasa kama hakuna hatua zilizochukuliwa mimi Mhe. Waziri ninafikiri mimi bado anieleze vizuri nitaendelea kulizuia hili fungu mpaka pale aniambie hatua gani atachukua basi kwa maofisa waliohusika na suala hili.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri chukua hatua ya kulishughulikia hili ili lisituweke hili jambo. Atachukua hatua kulifuatilia hili.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ninakushukuru Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwa kujadili wakati naomba mimi hoja yangu tusivutane sana na Mhe. Waziri kwa sababu katwambia mapema leo kwamba ni Ijumaa.

Mhe. Mwenyekiti, atakumbuka katika mchango wangu mimi nilikuwa mmoja niliyezungumzia kadhia ya wafanyakazi ambao yeye kawaita *freelance* ambao wapo pale katika redio, nikasema wengine wamepewa mikataba na wengine hawajapewa mikataba, kaniambia wanaendelea kufuata utaratibu wa kawaida.

Lakini labda watendaji wake hawakumsaidia Mhe. Waziri Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba ajira zilitoka, sasa kama hawa watu uliwaona hawana sifa unawatumiaje kwa misingi hiyo ndio ilikuwa hoja yangu. Wametumiwa wengine wana miaka miwili, mitatu, minne, mitano na wengine mpaka saba.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hawa hoja yao ni moja tu kwamba kumetangazwa nafasi tena lakini kwa utaratibu uliojengeka katika shirika hili Mhe. Waziri afahamu watendaji wake, wanatafuta watu nje wale waliokuwa wameshawatumikisha miaka yote, zikija ajira wanapewa jamaa zao na watu hao.

Sasa mimi kama nilivyosema sitaki kupoteza muda wa Mhe. Waziri, mimi naomba tu tukubaliane hapa ili tusipoteze muda kwamba nitampa haya majina ya hawa vijana 10 ambayo

ninayo na maelezo yao ili Mhe. Waziri akae na watendaji wake, mimi sina haja ya kuvutana naye akae na watendaji wake alifuatilie na pengine awatafute hawa, kwa sababu mara nyingi wanapokaa na watendaji peke yao wakubwa wao wanawapa taarifa, ninafikiri mara nyingi tunaowasaidia sisi Wawakilishi kuwapa taarifa Mhe. Waziri ambao watendaji wao huwa hawawapi taarifa kwa usahihi.

Kwa hivyo naomba haya majina nimkabidhi alifuatilie hili ili kama kuna haki yao, mimi ninamjua Mhe. Waziri ni moja ya mtu ambaye ana sifa ya kuwa Imamu hata katika sala ya Ijumaa kwa sababu ya uadilifu wake, kwa hivyo ninadhani hili atalisimamia vizuri ili tuhakikishe kwamba hawa vijana zinapotoka nafasi za ajira wanapewa nafasi kama wanavyopewa wenziwao.

Kama atanikubalia hilo Mhe. Mwenyekiti, mimi nitasema tuendelee bila ya kupoteza wakati.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, *concern* ya Mhe. Jussa inafanana na ile ya Mhe. Hamza, ninaahidi kwamba hiyo ajira ambayo itakayofanyika tutaisitisha kwanza na tutachukua majina hayo kama alivyosema Mhe. Hamza, na tutakaa na Mhe. Waziri anayeshughulikia Utumishi kuangalia kwamba hao vijana hali inaridhisha.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ninashukuru Mhe. Mwenyekiti, kwamba nitashirikiana naye na naomba tuendelee.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi nina jambo dogo sana hapa kwenye Idara hii Utangazaji.

Jana nilihoji kwamba wakati Mwenyekiti wangu wa kamati alipokuwa anatoa hotuba televisheni haikuonesha, baada ya kufuatilia nikaambiwa kwamba hakuna umeme. Lakini Masingini kuna jenereta maalum kwa ajili ya huduma ya umeme pale umeme unapokatika.

Lakini nikaambiwa kwamba hakuna betri na jenereta haijafanya kazi. Mhe. Waziri amekiri kwamba betri hakuna na jenereta haina kazi na amesema kwamba wameamua kuunda tume basi mpaka hili la betri iundwe tume. Maana yake tuchukue fedha za wananchi tuunde tume kwa betri na *service*. Kwa nini asimuondoshe yule ambaye hawezi kutafuta betri ya kukopa.

Mhe. Mwenyekiti, betri ni laki na ishirini, tuunde tume ya serikali ya wataalamu kwa betri, kwa nini tusimuondoshe yule akapelekwa Manispaa akafagia. Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nimeeleza kwa kina kweli kweli, hiyo na bado ninamueleza Mhe. Hija kwamba hatukuunda tume kwa ajili ya betri, Katibu Mkuu Kiongozi serikali imeunda tume kwa ajili ya kuangalia ufanisi mzima wa Shirika la ZBC. Hilo limekuja jana.

Lakini kukatika kwa matangazo si jambo geni kutokana na hali yetu hivi sasa. Tutajipanga kuona kwamba ufanisi unapatikana. Kwa hivyo sioni haya kusema hivi sasa Masingini sina laki nane ya kufanyia *service*.

Pemba hivi sasa Afisa Mdhamini amewajibika kukopa pesa kwenda kulipia umeme ili matangazo yapatikane. Juzi mimi nilikopa *AC* ya chumba cha matangazo. Kwa hivyo hali yetu ni hiyo, ukiwepo umeme Masingini matangazo yatapatikana kama haupo hatutoweza kuiba ili yapatikane matangazo.

Tutajihidi kwa kadri yetu yote baada ya bajeti hii kurekebisha mambo, ili wananchi wa Zanzibar waone televisheni yao masaa 24. Hilo ndilo ninalomuahidi lakini kwa hali ya hivi sasa kabla ya bajeti mpya kwa kweli nina uhaba mkubwa wa fedha katika Shirika langu la *ZBC*. Hayo ndio maelezo ninayoweza kusema.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimezungumza na mafundi ambao mwenyewe Mhe. Waziri ndio anaowatumia. Tatizo ni *service* na jenereta na betri. Ikiwa Wizara nzima haina uwezo wa kununua betri, mimi nitatoa betri Mhe. Mwenyekiti. Tusiwanyime Wazanzibari taarifa muhimu kwa sababu ya betri.

Mafundi wake wananiambia tatizo ni *service* na jenereta halina betri. Kwa hivyo Mhe. Waziri kama betri huna mimi *wallahi* nitakupa shilingi laki moja ishirini. Ni aibu kubwa kwa hivyo kama kuna watendaji hawawajibiki waondoke. Kwa hivyo Mhe. Waziri aniambie kuwa betri huna mimi nitakupa leo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Nimefurahi Mhe. Mwenyekiti, na nitakubali kuchukua shilingi laki nane kutoka kwa Mhe. Hija kwa ajili ya kufanya *service*.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi sikusema laki nane, nimesema pesa ya betri ni laki na ishirini na *service* nitachukua mimi nitatengeneza. Nime jenereta yako na betri nitakupa mimi nikatengeneze, kubali hilo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, tutajitahidi kufanya kila jitihada wiki moja hii tuliyonayo kuhakikisha kwamba tunapata pesa za betri na kufanya *service* pale.

Mhe. Mwenyekiti: Tunashukuru na mchango huo wa Mheshimiwa utasaidia sana katika uendeshaji ili tupate matangazo vizuri. Tunaendelea.

Ninadhani Mheshimiwa anapaswa kupongezwa sana kwa mchango huo mkubwa. Tunaendelea.

Kifungu 0704 Shirika la Utanganzaji Zanzibar, Unguja shs.161,194,000/=
Kifungu 1101 Idara ya Makumbusho

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilisema kuhusu ngoma zinazopigwa Ngome Kongwe. Kumekuwa na kutofahamiana

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe tumekosea kidogo kutoa idhini ya matumizi kwenye kifungu cha Pemba, hebu turudishe.

Kifungu 0704 Shirika la Habari Zanzibar, Unguja shs.1, 855,030,000/=

Kifungu 0705 Shirika la Utangazaji Zanzibar, Pemba shs.161, 194,000/=

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia jana nilisema kuhusu ngoma zinazopigwa Mji Mkongwe katika Ngome Kongwe kumekuwa na kutofahamiana na *signal tower* kwa ule mnara unaoongozea meli, ngoma zile zinapigwa kwa muda mrefu na nilimsikitikia sana Mhe. Waziri na Mhe. Jussa wa Jimbo la Mji Mkongwe alilizungumza kwa nguvu zote suala hili.

Mhe. Waziri tunaomba tuwasaidie wale jamaa ule mnara ni kitengo muhimu na zile ngoma uweze kuzisimamisha na leo ni Ijumaa.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mhe. Jaku na Mhe. Jussa walizungumzia suala la ngoma nyingi katika Mji Mkongwe.

Naomba radhi sikuweza kuwajibu suala hili kwamba sikuligusia kabisa. Ni kweli kwamba Mheshimiwa kumekuwa na mambo ambayo hayapendezi. Sisi serikalini suala hili tumeshalijadili mara nyingi na Mheshimiwa hata Juma Duni hapa naye ni mmoja anayelalamika sana.

Mhe. Makamo wa Kwanza kabla hajahama pale naye alikuwa anatulalamikia sana. Kwa hivyo tatizo hili tunalo si Mji Mkongwe tu. Kwa hivyo sisi katika wizara tumeamua kufanya hatua mbili.

Hatua ya kwanza kuiangalia sheria yetu na kitabu hiki tumeeleza kwamba tunatarajia kuifanyia marekebisho sheria inayohusiana na mambo ya sanaa, ili kuipa meno makali zaidi. Kwa hivyo hiyo ni hatua ya kwanza na tutajitahidi katika kikao ikiwezekana cha Januari basi suala hilo linaweza likaja.

Lakini la pili tumejaribu kuwaandikia barua wale wote ambao ni wapigaji wazuri wa ngoma, na wengine wameanza kukubaliana na sisi, wamepunguza kwa kiwango kikubwa. Sasa wale ambao hawajakubali basi naomba tushirikiane na Mhe. Jaku na Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Mji Mkongwe ili tuone kwamba bughudha wanayopata watu wetu inaondoka. Mhe. Mwenyekiti, jambo hili halipendezi kabisa.

Mhe. Mwenyekiti: Haya maelezo yanahusu jambo ambalo Mhe. Jaku pengine aliwahi tu lakini hapa tupo kwenye Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale.

Sasa wacha tupitishe hii na maelezo hayo yatakuwa yanahamishiwa huko sasa. Tuendelee.

Hiyo ya makumbusho sasa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Jaku kafanya haraka tu mimi nilikuwa ninasubiri katika Idara yake inayohusika, kwa sababu mimi ndiye muhusika hasa Mwakilishi wa Jimbo la Mji Mkongwe.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba nije katika Makumbusho na Mambo ya Kale jambo dogo tu. Mhe. Mwenyekiti, hili ninamuomba Mhe. Waziri lakini pia ikibidi Mhe. Waziri wa Nchi (0R) Utumishi wa Umma na Utawala Bora anisaidie.

Mhe. Mwenyekiti, nilihoji fungu la posho maalum katika idara hii kwamba ni ishirini na nne milioni laki sita na elfu kumi.

Hoja yangu nilisema kwamba fungu hili limekuwa linatupa tabu katika idara tofauti linakuwa na viwango tofauti za wizara tofauti Mhe. Mwenyekiti. Nimekuwa mfuatiliaji mzuri tangu tumeanza bajeti hii Waheshimiwa Mawaziri mashahidi kwamba fungu hili tumekuwa tukilihoji mara kwa mara.

Sasa tunapoambiwa katika idara mwenye kuhusika na posho maalum ni Mkurugenzi tu, tofauti na kwenye Idara ya Uendeshaji na Utumishi pale kunakuwa na Waziri, Naibu Waziri kama yupo, Katibu Mkuu lakini unashangaa kama serikali moja ambavyo viwango vyake vitakuwa vinafanana. Kila idara katika wizara tofauti ikija ina fungu linalotofautiana katika posho maalum.

Katika Wizara ya Kazi kulikuwa mara nyingi zinafanana, ilikuwa milioni kumi na moja, hapa angalau kidogo pana ukweli zote zinafanana lakini ilikuwepo moja ni milioni kumi na nne, kuna wizara nyengine milioni kumi na tano kwa mfano Wizara ya Katiba. Sasa Mhe. Mwenyekiti, hakuna ile *consistent* ndio inapotupa mashaka kwamba fedha hizi tofauti na maelezo wanayotoa Mawaziri kutujibu kwamba hizi ni kwa ajili ya posho zinazofuatana na mshahara ambapo mwaka jana ilikuwa inaunganishwa na mshahara, mwaka huu imetenganishwa. Lakini kama imetenganishwa mimi ninavyoamini kuwa sera ya serikali ya utumishi ya umma, wakurugenzi wote posho maalum yao itakuwa inalingana.

Sasa kwa nini wakurugenzi wa idara tofauti posho yao maalum inakuwa tofauti. Hii si kwamba kwa sababu unapewa *ceiling* kila kinachobakia kinatumbikizwa hapo watu wakatafune Mhe. Mwenyekiti. Naomba ufafanuzi mzuri wa suala hili niridhike kwamba mimi ninaamini kama kuna posho maalum la Mkurugenzi linapaswa kuwa sawa kwa wakurugenzi wote wa idara zote na wizara zote. Naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, posho maalum katika kifungu hiki si la Mkurugenzi peke yake na kwa kweli posho maalum katika idara halihusu Mkurugenzi tu, hutegemea katika idara kuna watu wangapi ambao ni *eligible* kupata posho maalum.

Hapo ndipo kinapanda na kushuka. Kwa hivyo posho maalum hapa kuna yeye mwenyewe Mkurugenzi, sekretari wake lazima apate, pana mwanasheria, kuna tarishi, dereva na karani wa masjala ya siri.

Sasa hutegemea na ukubwa wa idara, kuna wakati mwengine katika idara kuna watu hao lakini mwahali mwengine katika idara lakini hao wamekuwa *constant* kwenye ofisi moja. Kwa hivyo ndio ukaona yeye ana posho maalum yeye tu, lakini ukikuta idara ambapo imejiweka mbali

kama hii, hii haipo wizarani kwa hivyo hawa wengine hawamuhusu lakini ingelikuwa ipo wizarani lingepungua kwa sababu kuna hawa wengine wote wangefanya kazi moja.

Pale Wizarani pana watu ambao kama hao matarishi, mwanasheria huwa ni mmoja kwa wizara yote. Kwa hivyo huo ndio ufafanuzi ambao ninaoweza kuutoa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jussa uzingatie sana muda.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ninazingatia sana muda. Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru kwa ufafanuzi alionipa Mhe. Waziri lakini ninakumbuka na leo tunahimizwa sala ya Ijumaa.

Mhe. Mwenyekiti, nimeridhika na maelezo ya Mhe. Waziri lakini bado naomba kuna ahadi aliyotupa Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi Rais na Utumishi na wa Fedha kwamba baadae watatupatia Waheshimiwa Wajumbe maelezo ya hivi vifungu tuvielewe, kwa sababu kama nilivyosema na ingekuwa hatupati hoja hizi za wasi wasi ingekuwa Mawaziri wote wanaokuja wanatujibu sawa sawa.

Lakini kuna Waziri ukimuhoji anakwambia hili ni la Mkurugenzi tu, mwengine anakwambia la watendaji. Kwa hivyo ninasema hoja kama hizo tunazikubali kwa hoja kuwa baadae tutapewa maelezo ili na sisi turidhike kwamba fedha hizi zinatumika vizuri. Baada ya maelezo hayo naomba tuendelee, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Anachosema Mhe. Jussa kuwe na uwiano, kwa hivyo jambo hili lifanyiwe kazi kwa pamoja. Ninadhani tuendelee tunashukuru.

Kifungu 1101	Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale Unguja	457,320,000
Kifungu 1102	Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale Pemba	25,000,000

Kifungu 1201

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia fungu hili la Kamisheni ya Utamaduni na Michezo mbali na maelezo ya Mhe. Waziri mwenye kazi ile ile na *speed* mpya ya ari zaidi, kasi zaidi na nguvu zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, suala la uwanja wa amani, amelizungumza Mhe. Waziri, lakini katika maelezo yake amesema kwamba kwa kushirikiana na Rais mpya wa *ZFA* mwenye ari na uchu wa maendeleo ya soka Zanzibar. Lakini mbali na maelezi yake nilikuwa nataka kujua kwamba matayarisho hayo kwa kushirikiana na wadau na Rais mpya wa Zanzibar yataanza lini katika kufanyiwa ukarabati uwanja wa amani ili Wanzanzibari tuweze kutumia uwanja ule kwa ajili ya vilabu vyetu na mashindano yanayokuja ya miaka 50 ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, juzi niliona taarifa kwamba kuna wachezaji mastaa wa dunia wakiwemo Luwisfigo na Zenadine Zedan wanakuja Zanzibar. Je, wakija watacheza uwanja ule Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri atueleze uwanja ule utafanyiwa matengenezo kuanzia lini.

Mhe. Waziri wa Habari Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa najibu hoja hii nilisema kuna njia mbili tulizozipanga kushughulikia suala hili. Kuna za nje na za ndani. Hizo za ndani ndio ambazo zitaanza ghafla kwa sababu bahati mbaya Mhe. Raza hayupo, lakini tumeshakubaliana kwamba mara baada ya kikao hiki cha bajeti, tukae ofisini mimi, yeye na Rais Aman Makungu ambaye kweli ni kijana madhubuti, ambaye anapenda michezo na yuko *committed* kama alivyo Mhe. Raza, tutawashirikisha na wengine Mhe. Jaku pia aliomba kuingia ambaye ni mpenzi wa michezo tutamshirikisha na yeye, lakini kuona kwamba baada ya muda mfupi uwanja wetu wa michezo wa amani unaweza kuchezeka *match* ya kimataifa.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa maelezo mazuri ya Mhe. Waziri tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim ulikwisha hoja na maelezo yalitoka tukasema tuyahamishe kwa kuokoa muda. Enhe! Unasemaje kuhusu maelezo Mhe. Waziri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Tatizo sio suala hilo, kuna suala jengine ambalo linahusu kitengo hicho hicho Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia hoja hiyo.

Mhe. Mwenyekiti: Ile si ilikuwa inahusu hapa kwanza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hii ya mwanzo nafikiri keshanijibu Mhe. Waziri.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ni sanaa na muziki Zanzibar ambalo lina fungu lake.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hoja ya pili hii haina tatizo, Mhe. Waziri alizungumza mapema kabisa kuhusu klabu ya Malindi. Lakini bado imekuwa kizungu mkuti klabu ile kutaka kupangiwa ratiba. Mhe. Waziri najua hili ulilizungumza mapema aliuliza mwanamapinduzi suala hili katika kipindi cha maswali na majibu. Lakini bado watendaji wako wa ZFA timu hiyo hawataki kuipangia ratiba. Hebu Mhe. Waziri lifafanuwe hili bila ya kupoteza muda.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli sikumjibu suala, na sikumjibu kwa sababu baada ya amri ile ya mahakama, *ZFA* walikuwa wanaangalia katiba zao, katiba ya *TFF,* katiba ya *CECAFA* kwa namna ambavyo wasingeathiri shughuli zao. Kwa hivyo, niliwaagiza kwamba wakae pamoja na Baraza la Michezo na *ZFA* haraka sana kutoa maamuzi. Lakini wakati wanashughulikia hilo na wao Malindi wakaniletea barua, nikawaambia tulieni kidogo. Sasa bahati mbaya Malindi wakarudi tena mahakamani. Kwa hivyo, waliporudi mahakamani *ZFA* na wao ikabidi wakaitwa mahakamani,

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, suala likiwa mahakamani kwa mujibu wa kanuni zetu huwezi kulizungumza. Kwa hivyo, namuomba Mhe, Jaku Hashim Ayoub asubiri hizi mbio za Mahakama zikimaliza, halafu tutapata ufumbuzi wa kudumu. Lakini naogopa kulitia maneno ikaathiri utoaji wa haki mbele ya chombo hiki cha sheria.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hawa Malindi wamekwenda mahakamani baada ya kuwa ZFA hawataki kutekeleza tatizo hilo, ndio ikabidi Mionge akimbilie kule. Malindi hawana tatizo, yeye atakuwa tayari kwenda kuondosha mahakamani kesi hiyo. Lakini kwanza wapangiwe ratiba ili wakaondoshe mahakamani, hilo suala mimi nitalisimamia, yuko tayari Mhe. Waziri kwa hilo

Mhe. Mwenyekiti: Sasa jambo liko mahakamani, kama hamkufanya suluhu wenyewe mkaipeleka pale mahakamani likawa limeisha, basi sisi tutakuwa tuna uzito wa kuweza kuendelea nalo, kwa kuwa jambo lenyewe liko mahakamani. Ingekuwa mmekutana nje, halafu mkapeleka suluhu yenu kule mahakamani, wakaingiza ikawa ni sehemu ya maamuzi, basi jambo hili hapa lingekuwa rahisi. Lakini kwa kuwa

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hili suala haliko mahakamani, mahakama wameshatoa maamuzi tayari ZFA tu kutekeleza ndio waliokuwa hawataki kutekeleza, lakini suala limeshaondoka mahakamani.

Mhe. Mwenyekiti: kwa hivyo, limeshamaliza mahakamani au vipi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Limeshamaliza Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, mpaka jana mimi najua liko mahakamani. Sasa kama limeshamaliza taarifa hiyo sina. Kwa hivyo, waniletee hiyo *judgment* ya mahakama mimi nitafanya maamuzi haraka.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Sina tatizo mimi Mhe. Mwenyekiti, tuendelee. Nitamletea.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake kwa Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kwa sababu atakumbuka suala la Malindi hata mimi niliwasiliana naye na nikamkabidhi nyaraka zote ambazo klabu ya Malindi walikuwa wamenipatia na akaniahidi atalifuatilia ndio maana sikuliibua hapa, nilimpa heshima ya kufuatilia.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ilikuwa ni kuhusu mafungu ya matumizi katika Kamisheni ya Utamaduni na Michezo. Nilihoji vifungu vitatu vya kamisheni hii. Nashukuru kwamba nimepatiwa maelezo kwa baadhi yake. Namuomba Mhe. Waziri anisaidie kimoja ambachao hakukigusa kwenye maelezo yake, kiko katika ukurasa wa 635, kwenye fungu la matumizi mengineyo vote 282100, vote ndogo 282118 mikutano ya ushirikiano wa kimataifa. Atakumbuka Mhe. Waziri nilihoji kwamba kila mwaka kuanzia mwaka jana, kunaonekana kuna fungu kubwa la hii vote inayoitwa mikutano ya ushirikiano wa kimataifa yaani *Conference for International Cooperation.* Mwaka jana Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa 100,400,000, mwaka huu 115,000,000 nikataka maelezo kwamba imekusanywa aina gani hii ambayo inagharimu fedha kiasi kikubwa kama hicho. Nilikuwa naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Majibu kama ni mafupi toa ili tuombe kuongeza muda kidogo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti. Nilijibu kwamba fedha hizi ni kwa ajili ya kuvipa ruzuku vyama vyetu vinavyoshiriki katika mashindano mbali mbali ya kimataifa. Tumeweka hivi kwa sababu mara nyingi tunapata lawama kwamba vyama hivi hatuvifanyii haki kwa kuwapa pesa kidogo. Kwa hivyo, tumeongeza kidogo ili vyama hivi viweze kushiriki vizuri na kutuwakilisha vizuri Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwa maelezo hayo naridhika, nashukuru tuendelee.

(Hapa Baraza lilirudia kwa ajili ya kuongeza muda wa Baraza)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, samahani kidogo. Kwa kuwa hoja kuhusu kifungu hiki imekwisha, basi tukipitishe halafu turejee Baraza.

Kifungu 1201 Kamisheni ya Utamaduni na Michezo 767,400,000

(Hapa Baraza lilirudia kwa ajili ya kuongeza muda wa Baraza)

Mhe. Spika: Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

UTARATIBU

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, kwa kuwa kanuni zetu zinatuelekeza kwamba siku za Ijumaa tumalize shughuli zetu saa 6:00 kwa ajili ya shughuli maalum yaani ibada, na kwa kuwa napata wasi wasi kwamba Mhe. Waziri anataka kutuongeza muda ili tuweze kumaliza hii shughuli yetu, jambo ambalo linaweza likaakhirisha, ukiachia wenzetu wa Shiya ambao wanasali saa 8:00, inaweza ikaakhirisha shughuli zetu za ibada kwa sisi wenye madhehebu mengine.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mnasaba huo na kwa heshima kubwa na taadhima ya hali ya juu, naomba lizingatiwe hilo na Mhe. Waziri badala ya kuongeza muda, basi aliakhirishe hili Baraza hadi siku ya Jumatatu saa 3:00 kamili asubuhi, kusudi tuje tumalizie hii hoja.

Mhe. Spika: Sitaki nichukuwe maelekezo haya, kazi iliyobaki sio kubwa, sasa moja kati ya mawili Waheshimiwa Wajumbe tuamuwe. Nafikiri kazi iliyobaki kwa sababu ni ndogo, pengine dakika chache zinaweza zikatosha kumaliza. Vyenginevyo basi twende Ijumaa halafu turudi hapa tuje tumalize.

Hofu nyengine niliyonayo *quorum* kutokutimia wakati huo. Hivi sasa *quorum* tunayo. Mimi nadhani tumalize hii kazi. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa shughuli iliyokuwa mbele yetu imebakia kidogo kumalizika na kwa kuwa kwa muda wa kawaida kwa leo Ijumaa nao unamalizika, na kwa kuwa tunaweza kuimaliza shughuli hii na tukawahi Ijumaa, basi naomba Mhe. Spika, tuweke kanuni ya muda kando, ili tuweze kumaliza shughuli zetu kabla ya saa 6:30 na tuwahi Ijumaa. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Sasa Waheshimiwa Wajumbe, kwa kuwa tumeona mazingatio hayo mawili, basi tujitahidi sana tumalize muda mfupi, ili mambo yote mawili muhimu tuyawahi.

KAMATI YA MATUMIZI

Kifungu 1202	Baraza la Kiswahili	95,000,000
Kifungu 1203	Mchango wa *EACROTANAL*	21,000,000
Kifungu 1204	Baraza la Michezo la Taifa	

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nashukuru sana majibu ya Mhe. Waziri kuhusu kuuandaa ule mchezo ambapo akatuita pamoja na Makamu wa Pili wa Rais tukaweza kuangalia, halatu tupate kutoa muongozo. Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri aliangalie kwa undani zaidi hili suala kuliko hivyo alivyolifikiria.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia sasa hivi mchezo wa *kick boxer*, sio kama hauchezwi, huu mchezo unachezwa. Sisi tulikuwa tunacheza pale Kariakoo, kuna wengine walikuwa wanacheza Ngome Kongwe, kuna wengine wanacheza ngazi mia. Mhe. Mwenyekiti, wananchi wangu wengi wa Jimbo la Kwamtipura wanacheza Mivinjeni kule. Mhe. Mwenyekiti, mchezo huu unasaidia sana vijana kuwasaidia katika suala zima la ajira. Hivi sasa walinzi wengi badala ya kuchukuliwa wale watu wazima na gongo wakasinzia, wanachukuliwa vijana hawa ambao wanaweza kulinda hata bila ya gongo.

Mhe. Mwenyekiti, jengine vijana hawa wameshatuletea sifa mpaka za kimataifa wameshachukua medali. Sasa Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri ajaribu kuliangalia suala hili kwa upeo. Kwa hivyo, mimi nitashirikiana na Mhe. Waziri pamoja na hawa wahisani ambao wanafadhili mchezo huu, ili iandaliwe michezo minne mfululizo. Iandaliwe judo, ngumi, karati pamoja na *kick boxer*, halafu wao wenyewe watajaribu kuwaangalia. Halafu vile vile aangalie idadi ya watu watakaoingia katika mchezo ule, ili wajuwe kwamba mchezo huu unapendwa sana. Vyenginevyo mchezo huu kama hatujaukubali ndani ya sheria basi vijana wetu wengi watakuwa wanavunja sheria, kwa sababu mchezo unachezwa na vijana hawawezi kuuacha.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba Mhe. Waziri hebu ajaribu kuliangalia tena kwa upeo mkubwa zaidi katika suala zima la kutoa ajira, lakini pia na kujenga afya za vijana wetu. Mchezo wa kick boxer ndio niliokusudia zaidi, ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Hamza Hassan Juma kwa ushauri wake. Ndio kama nilivyosema kwamba naliangalia hili kwa undani zaidi na niko tayari kushirikiana naye katika kuangalia. Lakini tufanye baada ya Ramadhani bora, maana yake Ramadhani mtihani kidogo. Kwa hivyo, baada ya Ramadhani tufanye hivyo, halafu tutamshauri Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa busara, halafu tutowe

ushauri wa serikali kwa jumla katika kutoa maamuzi kwa maslahi ya vijana wetu. Hakuna tatizo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee. Namshukuru sana Mhe. Waziri.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimuunge mkono Mhe. Hamza Hassan kwa kuunga mkono suala hili la mchezo huu wa *kick boxer*. Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nachangia nilizungumza suala la vifaa vya mchezo wa *cricket* na Mhe. Waziri alisema kwamba vifaa vile vilikabidhiwa. Lakini taarifa ziliopo ni kwamba *TCA* ilikabidhi vifaa mara mbili. Je, makabidhiano hayo yalikuwa ni ya vifaa vya mara mbili.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, Bwana Juma Saadat hajatuambia hivyo. Kwa hivyo, labda mimi na yeye Mhe. Nassor Salim Ali, tumuone Mwenyekiti wa chama hiki, kama kuna matatizo yoyote tulifuatilie kwa undani zaidi, bila shaka tutapata ufumbuzi wake.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 1204 Baraza la Michezo la Taifa 147,000,000

Kifungu 1205

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, lakini kabla sijatoa hoja yangu nimuombe kwanza Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Wawi atutake radhi Shiha hatusali saa nane Ijumaa, kwa sababu hiki chombo ni kikubwa, hivyo sio vizuri kuchukua maneno ya mitaani ya pembeni ukayaingiza katika kumbukumbu rasmi za *Hansard* Mhe. Mwenyekiti. Nchi hii ina mjumuiko wa watu wa imani tofauti na wote chombo hiki kinapaswa kiwaheshimu na kutokufanya mzaha katika imani za watu wengine.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba yale maelezo ambayo niliyatoa mapema kuhusiana na suala la Baraza la Sanaa na Muziki, kuhusiana na suala la jumba la Ngome Kongwe kutumika kama ni kituo cha kupiga muziki hadi saa 8:00 au 9:00 za usiku, ambapo Mhe. Jaku Hashim Ayoub aliibua tukasema pahala pake hasa ni hapa.

Mhe. Mwenyekiti, nilimsikia Mhe. Waziri, sitaki kurefusha maelezo, nilishayasikia maelezo yake ya awali. Lakini kama nilivyomuambia katika mchango wangu, maelezo kama haya tumekuwa tukiyapata kila ninapotoa hoja hii, lakini baadae hakuna utekelezaji. Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani maelezo ya Mhe. Waziri yamejikita katika kuwaomba waliopiga ngoma. Mimi nadhani sio jukumu la serikali kuomba. Serikali ndio inayotoa kanuni juu ya matumizi ya maeneo tofauti, ni jukumu lake. Kwa hivyo, mimi nadhani katika hili badala ya kuomba tungoje mpaka wanaopiga ngoma wakubali. Mimi kama Mwakilishi wa Mji Mkongwe sitalikubali kabisa. Nililikubali mwaka jana, nikaliibua tena katika kamati mara kadhaa hapa katika ripoti zake, bado halipati ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba Mhe. Waziri aniambie kwamba atachukua hatua ya kuhakikisha, kwamba kwa kipindi hiki ambacho bado anashughulikia kutafuta mahala mbadala

pa kupiga shughuli kama zile. Kama nilivyosema ingekuwa ni shughuli za mwaka mara moja za ufunguzi wa matamasha zinazomalizikia saa 4:00 au 5:00. lakini miziki inaendelea kila wiki kwa siku za kazi na siku zilizokuwa sio za kazi, mpaka saa za usiku ni usumbufu mkubwa, kuna wazee, kuna watoto wadogo pale na kuna wanafunzi wanasoma wanahitaji utulivu wote hao wanaathirika.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri anipe kauli kwamba lini atahakikisha kwamba suala hili litafanyiwa kazi, kwa kuondosha pale na katika kipindi hiki ambacho analifanyia kazi ni kuondosha basi angalau kuwe na kanuni kwamba muziki utakaopigwa pale uwe hauzidi saa 5:00 za usiku Mhe. Mwenyekiti. Kama sijapata kauli hiyo basi fungu hili nitalizuwia leo hapa.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba binafsi nimetoa maelekezo, baada ya maelekezo ya serikalini kwamba suala hili linauthi na kwamba Katibu wa Baraza la Sanaa ameviandikia vilabu vyote ambavyo vinapiga muziki zaidi ya saa sita kwa siku hizo za Jumamosi. Kwa hivyo, labda nichukuwe wazo lake nikaiangalie kanuni na sheria iliopo, nguvu gani ninazo, halafu nitachukua hatua kwa hao, nakala kwa polisi Mkoa wa Mjini Magharibi na nakala kwake yeye mwakilishi, ili ajuwe kwamba tumechukua hatua.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nimesikia maelezo ya Mhe. Waziri, kama kawaida yangu ananijua kwamba ninapotoa hoja huwa sio mkaidi, lakini hili nimelisimamia kwa ukali huu kwa sababu kama nilivyosema, mimi kama Mwakilishi wao, basi wananchi wangu wananiona kama mimi silifanyii kazi hili na tumeshalizungumza sana.

Kwa hivyo, nasema nakubali ushauri alionipa na kwa sababu kama nilivyosema awali, namuheshimu sana Mhe. Saidi, naiona *seriousness* yake ya kazi tangu kaingia katika wizara hii, mabadiliko makubwa tumeyaona, naamini kwamba atalifanyia kazi, nitashirikiana naye, lakini nataka kuona kwamba suala hili linapatiwa ufumbuzi ili wananchi wangu wa maeneo ya Shangani Forodhani waachiwe wapumuwe.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, nakushukuru naomba tuendelee.

Kifungu 1205	Baraza la Sanaa na Muziki	42,000,000
Kifungu 1206	Bodi ya Sensa na Sinema	38,000,000
Kifungu 1207		

Mhe. Shadya Mohamed Suleiman: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikitoa mchango wangu, nilitaka kujua hatima ya kiwanja cha kufurahishia watoto kilichokua Chake Chake Pemba. Pamoja na majibu mazuri ya majumuisho ya Mhe. Waziri aliniambia kwamba kitashughulikiwa, kwa hivyo nilitaka kujua ni lini, kwa sababu muda umekuwa mrefu na watoto wetu wanataka kufurahi, ahsante.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli na nimuombe radhi Mhe. Mjumbe kwamba sikuweza kulijibu suala hili. Kwa hivyo, kwa kifupi

Mhe. Mwenyekiti, viwanja hivi vya kufurahishia watoto haviko tena wizarani kwetu, nilivirudisha katika Ofisi ya Mhakiki Mkuu wa Mali za Serikali, kwa hivyo hatuvisimamii tena sisi. Hivyo, hatuna mamlaka ya kuvizungumzia katika Baraza lako hili tukufu.

Mhe. Shadya Mohamed Suleiman: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Waziri anayeshughulikia ni nani hicho kiwanja.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, tumerudisha sisi katika Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, ambako ndiko kwenye Mhakiki Mkuu wa Mali za Serikali, mali yote ya serikali ambayo wizara kwa mujibu wa sheria ya manunuzi na ku-*deposit* mali ya serikali, basi niliirudisha kwao Wizara ya Fedha. Kwa hivyo, iko kule ambako inaweza kushughulikiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, juu ya maelezo mazuri aliyotoa Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, naomba kueleza kidogo ili tuweze kulielezea Baraza lako tukufu hili.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli anachosema Mhe. Shadya kwamba upo umuhimu wa kuwa na viwanja vya watoto, kwa ajili ya watoto wetu wanahitaji kufanya hivyo. Serikali imeshazungumza na shirika letu hili la *ZSSF* kwa nia ya kuendeleza viwanja vile kwa shughuli mbali mbali zikiwemo na michezo ya watoto. Kwa hivyo naomba Mhe. Shadya avute subra wakati serikali inashughulikia jambo hili, tunalielewa umuhimu wake na tunahitaji watoto wetu wapate mahala pa kuchezea kwa Unguja na Pemba Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Shadya Mohamed Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, naheshimu majibu ya Mhe. Waziri kama yangu Mhe. Mohammed Aboud, naomba tuendelee.

Kifungu 1207	Kamisheni ya Utamaduni na Michezo Pemba	45,000,000
	Jumla ya Fungu	**7,678,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na kamati ya matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 42 – WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, UTALII NA MICHEZO

Kifungu 0404	Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar	400,000,000
Kifungu 0702	Tume ya Utangazaji	100,000,000
Kifungu 1101	Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale	100,000,000
	Jumla ya Fungu	**600,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na kamati ya matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Hapa Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ilivyokua kamati ya matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya wizara yangu bila ya mabadiliko. Sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na makadirio hayo wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Nawashukuruni Waheshimiwa Wajumbe, kwa mashirikiano yenu makubwa katika kazi zetu hizi. Waheshimiwa Wajumbe kuna taarifa moja fupi kabla ya kuahirisha kikao hiki, kwamba Waheshimiwa Wawakilishi wa upande wa CCM wabaki kwa dakika chache sana humu ukumbini mara baada ya kuahirishwa kikao, dakika chache sana. Mnadhimu ametoa taarifa hiyo.

Baada ya hayo sasa Waheshimiwa Wajumbe, sasa naahirisha kikao hiki mpaka siku ya Jumatatu tarehe 30/07/2012 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 6:00 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 30/09/2012 saa 3:00 asubuhi)